**Rais** asema kifo cha Kwandikwa pigo kwa taifa
UKURASA 3



**Masharti** ya kunyonyesha ukipata corona
UKURASA 19



UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Agosti 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580662

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## KESI YA SABAYA

# Bosi wa Upelelezi apanda kizimbani

**SHAHIDI** ashangaa maelezo yake polisi kuwa tofauti, pungufu...

*Endelea ukurasa 2*



Walimu wawili wakifundisha katika darasa moja lenye wanafunzi wa madarasa tofauti, la pili na la tatu katika Shule ya Msingi Ifua, Kitongoji cha Ifua ambayo bado haijasajiliwa wilayani Kilolo, mkoani Iringa hivi karibuni. **PICHA: SILVANUS KIGOMBA**

# Mwendo wa chanjo kukabili baa corona

UKURASA 2




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa pili kulia), akikabidhi kwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. George Mulamula Tuzo ya Umahiri ya Euromoney kama Benki Bora Tanzania 2021 na Benki Bora kwa Huduma za Wateja Binafsi na Biashara, wakati wa hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi, Filbert Mponzi na Ofisa Mkuu wa Fedha, Juma Kimori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# Makalla asema barakoa lazima

UKURASA 3

**HABARI** | **MO FOUNDATION YAMWAGA MAMILIONI MUHIMBILI** UK. 19 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mwendo wa chanjo

**Na Waandishi Wetu**

SASA ni mwendo wa chanjo! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na kinachoshuhudiwa katika mikoa mbalimbali nchini kwa sasa, wakuu wa mikoa wakiongoza wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 kukabiliana na baa la corona.

Mkoani Mwanza jana, Mkuu wa Mkoa huo, Robert Gabriel, aliwaongoza mamia ya wananchi kupata chanjo hiyo kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Sekou Toure).

Akizungumza muda mfupi baada ya kupata chanjo hiyo jana, Gabriel aliwataka wananchi wote wanaohitaji kuchanjwa kufika katika vituo 27 vilivyotengwa kwa mkoa mzima.

Alisisitiza chanjo hiyo inatolewa kwa hiari na siyo lazima na wameanza na makundi ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 50, wenye matatizo ya magonjwa sugu yakiwamo kisukari, shinikizo la damu, sikoseli, moyo na mengine.

Alisema wataalamu wamethibitisha kwamba chanjo hiyo ni salama kwa matumizi ya afya na kuwataka kuondoa uoga uliojengeka kwa baadhi ya wananchi.

Gabriel alisema licha ya Tanzania kupata chanjo na wananchi wake kuanza kuchanjwa, watu waendelee kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka na kuchukua tahadhari zote za kujikinga.

Viongozi wengine waliochanjwa jana ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, Antony Diallo, na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi.

Vilevile wananchi wakiwamo wazee, watumishi wa sekta ya afya, wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza walipata fursa hiyo ya kuchanjwa.

ARUSHA

Jijini Arusha, Nipashe jana ilishuhudia mwitikio mkubwa wa wananchi kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (AICC) ambao ulitumika kwa uzinduzi wa chanjo hiyo kimkoa.

Mmoja wa wananchi hao, Anita John, alisema kuwa jana ilikuwa siku muhimu kwake na baada ya kupata chanjo hiyo, atahamasisha wenzake wanaosita kupata chanjo hiyo.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alikuwa miongoni mwa viongozi waliojitokeza kupata chanjo mkoani Arusha.

Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongela, alisema chanjo hiyo inatakiwa wachomwe watu wenye umri zaidi ya miaka 18 na kipaumbele zaidi kwa sasa ni watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka 50.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Mosses Mzuna, alisema majaji ndio waamuzi wa kesi mbalimbali ili kuziamua vizuri ni lazima kila mmoja awe na afya iliyo bora.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Shaaban Juma, alisema ni wajibu wa viongozi wa dini kushirikiana na serikali kuelimisha waumini wao kuhusu upotoshaji dhidi ya chanjo hiyo.

Mkoani Kilimanjaro kumetolewa onyo kwa watumishi wa umma watakaotoa chanjo kwa upendeleo.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa huo NA Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Said Mtanda, alisema hawatamvumilia watumishi watakaoendekeza undugu na kupendelea.

"Leo (jana) tunazindua zoezi hili katika Kituo cha Afya Majengo, lakini tutatembelea na kujionea hali ya utoaji wa huduma katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, Hospitali ya Rufani ya Kanda (KCMC) na Kituo cha Afya Pasua. "Matatizo madogo madogo hayakosekani, ila tunayafanyia kazi katika kuakikisha zoezi hili linaendelea vizuri na kwa wakati.


"Mkoa wetu umetengewa dozi za chanjo 60,000 hadi leo (jana) tayari zimeletwa dozi 10,000, katika Wilaya ya Moshi tumepokea dozi 2700, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mawenzi) tutaweka dozi 500, KCMC 500, hii ni awamu ya kwanza, kesho na keshokutwa tutapokea dozi nyingine," alisema.

Uzinduzi wa chanjo kimkoa pia ulishuhudiwa jana katika mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita alizindua chanjo hiyo kitaifa na yeye mwenyewe kuchanjwa, ili kuonyesha jamii kwamba yuko tayari kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19, ambao bado unasumbua dunia.

Baada ya Rais Samia yalifuata makundi mbalimbali ya serikali wakiwamo mawaziri, waandishi wa habari, wakuu wa mikoa na wilaya, watumishi wa Sekta ya Afya na wananchi wa kawaida.

**■Imeandikwa na Richard Makore (MWANZA), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Mary Mosha (MOSHI), Renatha Msungu na Ibrahim Joseph (DODOMA).**



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, akipatiwa chanjo ya ugonjwa wa corona katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure, jana. **PICHA: RICHARD MAKORE**

# Bosi wa upelelezi atinga kizimbani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Upelelezi Wilaya ya Arusha, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Gwakisa Minga, amepanda kizimbani kutoa ushahidi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Wakati Minga akipanda kizimbani, shahidi wa sita wa Jamhuri, katika kesi hiyo, Bakari Msangi (38), ameeleza kushangazwa na maelezo aliyotoa polisi kuandikwa tofauti wakati akihojiwa kuhusu tukio la kupigwa, kutekwa nyara na kuporwa Sh. 390000.

Akitoa ushahidi wake, Minga (45) alidai kwamba kitendo cha kuvamia duka la Mohamed Saad, kilichofanywa ni kinyume cha sheria kwa kuwa mshtakiwa huyo, hakuwa na kibali chochote cha kwenda kufanya tukio katika eneo hilo.

Minga mkazi wa Sakina jijini Arusha, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, alidai kwamba Februari 9, mwaka huu, majira ya saa 4:00 usiku alikuwa Kituo cha Polisi Arusha, wakati akiendelea na majukumu yake, alipigiwa simu na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi.

Alidai kwamba Kihongosi alimweleza kwamba Sabaya amekamata watuhumiwa, hivyo kama walikuwa na shauri la kijinai upelelezi uendelee na kama halikuwapo ampatie mrejesho. Alidai kwamba Kihongosi hakumweleza watuhumiwa hao wamekamatwa wapi na kwa makosa gani.

Baada ya kupokea taarifa hizo, alimjulisha Mkuu wa Polisi Wilaya ya Arusha (ASP Muchunguzi) na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha (ACP Mwafulambo) na walimweleza kwamba asubiri Sabaya afike polisi na watuhumiwa hao na afanye mahojiano nao.

"Baada ya muda mfupi, Sabaya alifika kituo cha polisi wakiwa na vijana wawili ambao sikuwahi kuonana nao tofauti na siku hiyo. Sabaya alipofika na vijana hao, alidai kwamba aliwakamata kwa kosa la uhujumu uchumi na nilimhoji kuwa anipe uthibitisho kama kuna sehemu aliyofungua kesi na pili nilimtaka Sabaya kuandika maelezo yake kituo cha polisi lakini alikataa.

"Jambo la tatu baada ya kusikiliza maelezo yake, niliona kitendo alichokifanya ni kinyume cha sheria za nchi kwa sababu utaratibu haukufuatwa kwa kuwa aliingia kwenye nyumba ya mtu bila kuwa na kibali," alidai.

Shahidi huyo alidai baada ya kufanya mahojiano, alibaini kwamba Sabaya aliwakamata vijana hao kwenye duka la Mohamed Saad.

"Ukiangalia tukio hilo hapakuwapo na vyombo vingine vya dola na operesheni hiyo haikuwa ikitambuliwa na Jeshi la Polisi na hakukuwapo kwa taarifa yoyote, hivyo mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) alikuwa na nia ovu," aliendelea kudai.

Pia alidai kuwa vijana hao walipofika kituoni huko, walikuwa na mwonekano wa kupigwa kwa kuwa walikuwa na alama usoni na kwenye mashavu.

"Baada ya kukamilisha mahojiano na Sabaya nilijiridhisha kwamba hakukuwa na kosa na utaratibu pia mshtakiwa wa kwanza aligoma kuandika maelezo. Sabaya aliondoka na sisi tuliendelea kuwahoji Numan na Hajirini na tulishindwa kumkamata Sabaya kwa kuwa alikuwa na mamlaka ni mteule wa Rais, hivyo baada ya upelelezi kukamilika ndio tunapeleka ushahidi kwa mamlaka iliyomteua badala ya kumkamata na huo ndio utaratibu wa kipolisi," alidai.

"Baada ya kuwahoji Hajirini na Numan, tulibaini kwamba vijana wale walivamiwa, wamepigwa sana na kuporwa fedha na Sabaya akiwa na walinzi wake.

"Sabaya mamlaka yake yalikuwa yapo Hai na kabla ya kufanya tukio hilo alipaswa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola vya Arusha. Huo ndio utaratibu wa kisheria unaotambulika lakini Sabaya baada ya kufanya tukio hilo ndipo alitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya wakati ni makosa kisheria," aliongeza kudai.

Aidha shahidi huyo, alidai kwamba Sabaya, aliwasiliana na Kenani Kihongosi, baada ya kuwakamata vijana hao akimwomba wahifadhiwe katika kituo chetu cha polisi.

Katika hatua nyingine, Shahidi wa sita wa Jamhuri, katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amedai kwamba ameshangazwa na maelezo ya polisi kuandikwa tofauti wakati akihojiwa kuhusu tukio la kupigwa, kutekwa nyara na kuporwa Sh. 390,000.

Shahidi huyo, Bakari Msangi(38), alielezea kushangaa baada ya kusomewa maelezo aliyoandika kituo cha polisi kutofautiana na kile alichozungumza na kukitolea ushahidi mahakamani.

Alidai maelezo ya polisi yametofautiana na kile alichotoa katika ushahidi wake sambamba na nyaraka zilizowasilishwa mahakamani kuwa pungufu.

Pia alidai kwamba alisainishwa maelezo hayo kwa kuwa alikuwa na maumivu hivyo alitaka kwenda kutibiwa na kwamba hakusomewa kabisa kilichoandikwa na askari aliyechukua maelezo.

Sambamba na hayo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, ambako kesi hiyo inasikilizwa, jana iliridhia ombi la mawakili wa utetezi la kusomwa maelezo yaliyoandikwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Arusha na 38 kama kielelezo cha kutikisa ushahidi wake, alioutoa mahakamani na maelezo ya awali ya polisi.

Awali, mawakili wa utetezi, walidai mahakamani hapo kwamba ushahidi uliotolewa mahakamani na shahidi huyo unatofautiana na maelezo yo awali aliyoandika polisi.

Hata hivyo, mawakili wa Jamhuri walipinga ombi la utetezi kwa madai kuwa maelezo yalioyandikwa na shahidi kituo cha polisi si sahihi kwa kuwa shahidi hakusomewa bali alisainishwa na askari aliyekuwa akichukua maelezo.

## HABARI KITAIFA

# Rais asema kifo cha Kwandikwa ni pigo

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema taifa limepoteza mtu muhimu kutokana na kifo cha Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa.

Waziri huo alifikwa na umauti juzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa akitibiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffer Haniu, Rais Samia ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, kutokana na kifo hicho.

"Tumepoteza mtu muhimu ambaye mchango wake katika utumishi wa umma hautasahaulika. Kwandikwa alikuwa kiongozi shupavu ambaye alikuwa akitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria na taratibu," Rais Samia alikaririwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.

Mkuu wa Nchi alimtaka Jenerali Mabeyo kufikisha salamu zake za pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na watu wote waliguswa na msiba huo.

Chama Cha Mapinduzi (CCM) pia kimetuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha mbunge huyo wa Ushetu mkoani Shinyanga.

Katika salamu za chama hicho jana, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema wamepokea kwa masikitiko taarifa za kifo hicho.

Alisema Kwandikwa alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa katika Wilaya ya Kibaha mwaka 2012 hadi mwaka 2015, Kahama mwaka 2015 mpaka sasa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Shinyanga mwaka 2015 na Mbunge wa Ushetu kutoka mwaka 2015 hadi 2021.

Pia alikuwa Naibu Waziri wa Ulinzi, Uchukuzi na Mawasiliano mwaka 2017 hadi mwaka 2020 na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi umati unamfika.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, pia ilibainisha Spika Job Ndugai amepokea kwa mshtuko na masikitiko taarifa ya kifo cha waziri huyo.

"Ninatoa pole kwa serikali, waheshimiwa wabunge, familia na wananchi wa Jimbo la Ushetu, Mwenyezi Mungu awape moyo wa ustahimilivu na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu," Spika Ndugai alikaririwa katika taarifa hiyo.

Alisema taarifa zaidi zitatolewa baada ya ofisi kupata utaratibu na ratiba ya mazishi kutoka serikalini.

■**Imeandikwa na Romana Mallya, Haika Christopher na Sechellah Nakamba (SJMC).**




Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, wakiwa mbele ya gari aina ya Volkswagen, baada ya kutembelea kwenye kiwanda cha kutengenezea magari cha CFAO Motors, jijini Kigali nchini Rwanda jana. **PICHA: IKULU**

# Makalla asisitiza uvaaji barakoa na 'level seat'

**Na Maulid Mmbaga**

HUKU tahadhari ya corona ikionekana kutozingatiwa kwenye maeneo mengi mkoani Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, amesisitiza uvaaji wa barakoa kwenye vyombo vya usafiri na 'level seat' ni lazima.

Jana, kiongozi huyo alisisitiza utekelezaji wa agizo lake hilo, akizitaka mamlaka ikiwamo ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwaelekeza makondakta kulisimamia.

Aliiambia Nipashe jana kuwa juzi alikutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na kupitia tathmini ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya juu ya kujikinga na UVIKO-19 na kuendelea kusisitiza suala la 'level seat' na kuvaa barakoa kuwa ni lazima.

Pia aliagiza LATRA na wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwaelekeza madereva na makondakta wa daladala kuhakikisha wanasimamia agizo hilo la 'level seat' na kuepuka kubeba abiria asiyevaa barakoa.

"Ninarudia tena, sasa sio hiari kuvaa barakoa kwa mtu anayeingia kwenye daladala, kivuko au mwendokasi, ni lazima na ni sharti, nimefanya utafiki katika vivuko mtu anaingia na barakoa kwa sababu tu kuna usimamizi, akifika ndani anavua, anapotaka kutoka anaivaa, unapovaa barakoa unajikinga wewe na unamkinga mwenzako.

"Niwatake wasimamizi iwe Feri, wamiliki, madereva na makondakta, na watu wote wanaohusika na vyombo vya usafiri kuhakikisha kwamba kuna 'level seat', maji ya kunawia mikono na mtu aingie kukaa kwenye 'seat' akiwa na barakoa," alisisitiza.

Aliongeza kuwa katika kutekeleza agizo hilo madereva na makondakta wawaangalie wanafunzi wasiendelee kunyanyasika kwa kuwaruhusu kuingia angalau watano lakini wakiwa wamevaa barakoa.

"Niwaombe wananchi, huvai barakoa au hunawi ili kumridhisha mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya au mamlaka husika inayosimamia jambo hili, ni kwa usalama wako, hali katika mikoa mingine na nchi jirani sio nzuri," alionya.

Nipashe ilishuhudia jana kwenye maeneo mbalimbali yakiwamo masoko na daladala jijini, wananchi wakiwa hawajavaa barakoa huku 'level seat' nayo ikionekana mtihani kwenye daladala.

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by:
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

**EU-EAC Market Access Upgrade Programme (MARKUP)**

**TENDER INVITATION**
**FOR**
**GENERATION OF TOTAL ASH, IRON, COPPER AND CADMIUM DATA FOR COCOA BEANS, COCOA POWDER AND COCOA BUTTER IN TANZANIA**

The East African Community (EAC) in partnership with the European Union, through the Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ), is implementing an initiative to enhance access of coffee, tea, cocoa, spices, oilseeds and horticultural produce value chains to the European union (EU) market and beyond. The initiative is called EU-EAC Market Access Upgrade Programme (MARKUP) and one of its key objectives is to improve harmonization of East African (EA) Standards of commodities in the priority value chains. To achieve this objective, MARKUP is supporting the EA Standards Technical Committees (EAS TCs) to upgrade the existing EA standards of these priority commodities with the current requirements set by the Codex Alimentarius Commission (Codex) and the EU.

Currently, the maximum limits (MLs) for contaminants in the EA standards are based on Codex Standards. Consequently, any contaminant that is not regulated by Codex is unlikely to be included in the EA standards. A meeting of the EAC TC on coffee, cocoa and related products held in November 2020, requested GIZ to support generation of data on the occurrence of ash and cadmium in cocoa powder or iron and copper in cocoa butter. Likewise, a meeting of the EAC Codex Forum held in March 2021, discussed the setting of a maximum limit (ML) for cadmium in cocoa powder to inform national positions at the 14th meeting of the Codex Committee on Contaminants in Foods (CCCF14) and agreed that there was a need to generate data on cadmium contamination in cocoa beans from the EAC region. The data are needed to perform exposure assessment and evaluate appropriateness of proposed limits.

It is in this context, EAC secretariat, through GIZ wishes to partner with an expert in Tanzania to assess the contents of ash, iron and copper and cadmium in cocoa and cocoa products in this country. Tanzania is one of the two main cocoa producing countries in the EA region.

The experts are expected to provide the requested service from August - October 2021. GIZ invites experts with relevant proven record and expertise in conducting similar assignments to submit their applications.

**Interested candidates should request for detailed tender documents from giz-tanzania@giz.de** no later than **10th August 2021.**

**The advert is solely intended for Tanzania Appraisers only.**

216391002

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## KUMB: PPR/2021 - 08/1

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 AGOSTI 2021

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, tarehe 4 Agosti 2021.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Julai 2021. Kwa Agosti 2021, bei ya rejareja ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 21/Lita (sawa na asilimia 0.89), Shilingi 36/lita (sawa na asilimia 1.63) na Shilingi 55/lita (sawa na asilimia 2.58), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 21.29/Lita (sawa na asilimia 0.94), Shilingi 36.06/lita (sawa na asilimia 1.73) na Shilingi 54.52/lita (sawa na asilimia 2.74), mtawalia.

(b) Kwa mwezi Agosti 2021, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimeongezeka ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 1 Julai 2021. Kwa mwezi Agosti 2021, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 38/lita (sawa na asilimia 1.53) na shilingi 79/lita (sawa na asilimia 3.54), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 37.43/lita (sawa na asilimia 1.61) na shilingi 79.12/lita (sawa na asilimia 3.74) mtawalia. *Kutokana na kuisha kwa Mafuta ya Taa kwenye matanki ya kuhifadhia yaliyopo Tanga, waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kuchukua mafuta ya Taa kutoka katika mkoa wa Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea Mafuta ya Taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*

(c) Kwa mwezi Agosti 2021, bei za rejareja na jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)** zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 1 Julai 2021. Kwa mwezi Agosti 2021, bei za rejareja za Petroli zimepungua kwa shilingi 22/lita (sawa na asilimia 0.92) na bei ya Dizeli imeongezeka kwa shilingi 24/lita (sawa na asilimia 1.05). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimepungua kwa shilingi 22.30/lita (sawa na asilimia 0.97) na bei ya Dizeli imeongezeka kwa shilingi 23.60/lita (sawa na asilimia 1.11).

(d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (BPS Premium).

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166,** bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo *(price cap)* kama ilivyokokotolewa na kanuni *(formula)* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP *(Electronic Fiscal Pump Printers)* na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| Dar es Salaam | 2,427 | 2,251 | 2,176 |
| Arusha | 2,543 | 2,380 | 2,260 |
| Arumeru (Usa River) | 2,543 | 2,380 | 2,260 |
| Karatu | 2,561 | 2,399 | 2,278 |
| Longido | 2,554 | 2,391 | 2,271 |
| Monduli | 2,548 | 2,386 | 2,265 |
| Monduli-Makuyuni | 2,553 | 2,390 | 2,270 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,627 | 2,465 | 2,351 |
| Coast (Kibaha) | 2,431 | 2,256 | 2,180 |
| Bagamoyo | 2,438 | 2,263 | 2,187 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,469 | 2,293 | 2,217 |
| Chalinze Junction | 2,441 | 2,266 | 2,190 |
| Chalinze Township (Msata) | 2,445 | 2,270 | 2,194 |
| Kibiti | 2,447 | 2,272 | 2,196 |
| Kisarawe | 2,434 | 2,259 | 2,183 |
| Mkuranga | 2,437 | 2,261 | 2,185 |
| Rufiji | 2,454 | 2,279 | 2,203 |
| Dodoma | 2,486 | 2,310 | 2,234 |
| Bahi | 2,493 | 2,318 | 2,242 |
| Chamwino | 2,481 | 2,306 | 2,230 |
| Chemba | 2,512 | 2,337 | 2,261 |
| Kondoa | 2,518 | 2,343 | 2,267 |
| Kongwa | 2,483 | 2,308 | 2,232 |
| Mpwapwa | 2,487 | 2,311 | 2,236 |
| Mtera (Makatopora) | 2,504 | 2,329 | 2,253 |
| Mvumi | 2,492 | 2,317 | 2,241 |
| Geita | 2,592 | 2,417 | 2,341 |
| Bukombe | 2,581 | 2,406 | 2,330 |
| Chato | 2,613 | 2,438 | 2,362 |
| Mbogwe | 2,630 | 2,455 | 2,379 |
| Nyang'hwale | 2,607 | 2,432 | 2,356 |
| Iringa | 2,491 | 2,316 | 2,240 |
| Ismani | 2,496 | 2,321 | 2,245 |
| Kilolo | 2,495 | 2,320 | 2,244 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,501 | 2,326 | 2,250 |
| Mufindi (Igowole) | 2,510 | 2,334 | 2,258 |
| Kagera (Bukoba) | 2,642 | 2,467 | 2,391 |
| Biharamulo | 2,617 | 2,441 | 2,365 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,659 | 2,483 | 2,408 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,664 | 2,489 | 2,413 |
| Muleba | 2,642 | 2,467 | 2,391 |
| Ngara | 2,630 | 2,455 | 2,379 |
| Misenyi | 2,651 | 2,475 | 2,400 |
| Katavi (Mpanda) | 2,635 | 2,460 | 2,384 |
| Mlele (Inyonga) | 2,654 | 2,479 | 2,403 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,628 | 2,452 | 2,377 |

216391702

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tanganyika (Ikola) | 2,653 | 2,477 | 2,402 |
| Kigoma | 2,658 | 2,483 | 2,407 |
| Uvinza (Lugufu) | 2,670 | 2,495 | 2,419 |
| Buhigwe | 2,647 | 2,472 | 2,396 |
| Kakonko | 2,615 | 2,440 | 2,364 |
| Kasulu | 2,644 | 2,469 | 2,393 |
| Kibondo | 2,623 | 2,447 | 2,371 |
| Kilimanjaro (Moshi) | 2,532 | 2,370 | 2,249 |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,536 | 2,373 | 2,253 |
| Mwanga | 2,525 | 2,363 | 2,242 |
| Rombo (Mkuu) | 2,549 | 2,387 | 2,270 |
| Same | 2,519 | 2,356 | 2,236 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,539 | 2,377 | 2,256 |
| Lindi | 2,422 | 2,289 | 2,235 |
| Lindi-Mtama | 2,426 | 2,294 | 2,253 |
| Kilwa Masoko | 2,445 | 2,313 | 2,209 |
| Liwale | 2,457 | 2,325 | 2,255 |
| Nachingwea | 2,441 | 2,309 | 2,264 |
| Ruangwa | 2,448 | 2,315 | 2,265 |
| Manyara (Babati) | 2,577 | 2,414 | 2,298 |
| Hanang (Katesh) | 2,587 | 2,425 | 2,309 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,592 | 2,430 | 2,309 |
| Mbulu | 2,590 | 2,427 | 2,311 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,609 | 2,446 | 2,330 |
| Mara (Musoma) | 2,605 | 2,430 | 2,354 |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,646 | 2,471 | 2,395 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,614 | 2,439 | 2,363 |
| Rorya (Shirati) | 2,649 | 2,474 | 2,398 |
| Bunda | 2,597 | 2,421 | 2,345 |
| Bunda (Kisorya) | 2,606 | 2,431 | 2,355 |
| Butiama | 2,602 | 2,427 | 2,351 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,651 | 2,476 | 2,400 |
| Tarime | 2,616 | 2,441 | 2,365 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,621 | 2,446 | 2,370 |
| Mbeya | 2,534 | 2,359 | 2,283 |
| Chunya | 2,543 | 2,368 | 2,292 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,549 | 2,373 | 2,298 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 2,551 | 2,375 | 2,299 |
| Kyela | 2,550 | 2,374 | 2,299 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,518 | 2,343 | 2,267 |
| Rujewa (Madibira) | 2,531 | 2,356 | 2,280 |
| Rujewa (Kapunga) | 2,528 | 2,353 | 2,277 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,543 | 2,368 | 2,292 |
| Morogoro | 2,452 | 2,277 | 2,201 |
| Mikumi | 2,467 | 2,292 | 2,216 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,490 | 2,314 | 2,238 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,512 | 2,337 | 2,261 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,501 | 2,326 | 2,250 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,500 | 2,325 | 2,249 |
| Malinyi | 2,511 | 2,335 | 2,259 |
| Kilosa | 2,470 | 2,295 | 2,219 |
| Gairo | 2,470 | 2,295 | 2,219 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,462 | 2,287 | 2,211 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,452 | 2,277 | 2,201 |
| Turian | 2,477 | 2,302 | 2,226 |
| Mtwara | 2,408 | 2,275 | 2,248 |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,444 | 2,312 | 2,297 |
| Masasi | 2,424 | 2,291 | 2,274 |
| Newala | 2,429 | 2,296 | 2,280 |
| Tandahimba | 2,422 | 2,289 | 2,273 |
| Nanyamba | 2,422 | 2,289 | 2,273 |
| Mwanza | 2,577 | 2,402 | 2,326 |
| Kwimba | 2,595 | 2,420 | 2,344 |
| Magu | 2,585 | 2,410 | 2,334 |
| Misungwi | 2,571 | 2,396 | 2,320 |
| Sengerema | 2,609 | 2,434 | 2,358 |
| Ukerewe | 2,636 | 2,461 | 2,385 |
| Njombe | 2,519 | 2,344 | 2,268 |
| Njombe (Kidegembye) | 2,540 | 2,365 | 2,289 |
| Ludewa | 2,557 | 2,382 | 2,306 |
| Makambako | 2,512 | 2,336 | 2,260 |
| Makete | 2,550 | 2,375 | 2,299 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,517 | 2,342 | 2,266 |
| Rukwa (Sumbawanga) | 2,600 | 2,424 | 2,349 |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,600 | 2,424 | 2,349 |
| Kalambo (Matai) | 2,607 | 2,432 | 2,356 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,613 | 2,438 | 2,362 |
| Ruvuma (Songea) | 2,493 | 2,361 | 2,299 |
| Mbinga | 2,506 | 2,373 | 2,333 |
| Namtumbo | 2,484 | 2,352 | 2,328 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,531 | 2,399 | 2,343 |
| Tunduru | 2,459 | 2,326 | 2,358 |
| Shinyanga | 2,556 | 2,381 | 2,305 |
| Kahama | 2,569 | 2,394 | 2,318 |
| Kishapu | 2,584 | 2,409 | 2,333 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,587 | 2,412 | 2,336 |
| Salawe | 2,570 | 2,395 | 2,319 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,597 | 2,422 | 2,346 |
| Busega (Nyashimo) | 2,590 | 2,415 | 2,339 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,600 | 2,425 | 2,349 |
| Maswa | 2,589 | 2,413 | 2,337 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,596 | 2,420 | 2,345 |
| Singida | 2,518 | 2,342 | 2,266 |
| Iramba | 2,530 | 2,354 | 2,278 |
| Manyoni | 2,502 | 2,327 | 2,251 |
| Itigi (Mitundu) | 2,518 | 2,342 | 2,266 |
| Ikungi | 2,513 | 2,338 | 2,262 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,542 | 2,367 | 2,291 |
| Songwe (Vwawa) | 2,543 | 2,368 | 2,292 |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,550 | 2,375 | 2,299 |
| Ileje | 2,547 | 2,372 | 2,296 |
| Momba (Chitete) | 2,552 | 2,377 | 2,301 |
| Tunduma | 2,547 | 2,372 | 2,296 |
| Tabora | 2,535 | 2,360 | 2,284 |
| Igunga | 2,535 | 2,360 | 2,284 |
| Kaliua | 2,548 | 2,373 | 2,297 |
| Ulyankulu | 2,545 | 2,370 | 2,294 |
| Nzega | 2,545 | 2,370 | 2,294 |
| Sikonge | 2,544 | 2,369 | 2,293 |
| Urambo | 2,545 | 2,370 | 2,294 |
| Uyui | 2,541 | 2,366 | 2,290 |
| Mpyagula | 2,567 | 2,391 | 2,315 |
| Tanga | 2,486 | 2,324 | 2,222 |
| Handeni | 2,507 | 2,344 | 2,201 |
| Kilindi | 2,522 | 2,359 | 2,236 |
| Korogwe | 2,498 | 2,336 | 2,215 |
| Lushoto | 2,508 | 2,345 | 2,224 |
| Mkinga (Maramba) | 2,493 | 2,331 | 2,236 |
| Muheza | 2,491 | 2,329 | 2,222 |
| Pangani | 2,493 | 2,330 | 2,228 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 2,297.20 | 2,122.07 | 2,047.04 |
| TANGA | 2,356.26 | 2,194.08 | - |
| MTWARA | 2,278.45 | 2,145.83 | |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

216391702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakurugenzi wapya halmashauri watambue nafasi zao ni dhamana

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alifanya uteuzi wa wakurugenzi wa halmashauri za majiji, manispaa miji na wilaya 184 miongoni mwao wakiwa wapya na wengine kuhamishwa vituo vya kazi.

Jambo hilo lilisubiriwa kwa muda mrefu kutokana na uteuzi mbalimbali ambao Rais amekuwa akiufanya tangu aingie madarakani machi 19, mwaka huu, baada ya aliyekuwa Rais John Magufuli, kufariki dunia. Alianza kumteua Katibu Mkuu Kiongozi, kupangua baraza la mawaziri, makatibu wakuu wa wizara, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na baadaye wakuu wa wilaya.

Katika uteuzi huo, ambao walioteuliwa walitakiwa kuripoti vituo vyao vya kazi jana, kama ilivyo ada inapotokea hali kama hiyo, kuna wanaoendelea na wengine kuachwa pamoja na sura mpya kuchomoza, ndivyo ilivyotokea baada ya wakurugenzi 54 kutumbuliwa.

Aidha, wakurugenzi hao walioteuliwa, 70 walihamishwa vituo vya kazi na 45 wamebaki katika vituo vya awali. Kadhalika, 69 ni wapya wakiwamo 15 walioteuliwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi baada ya waliokuwa wakishikilia nafasi hizo uteuzi wao kutenguliwa.

Licha ya kwamba hakuna sababu zilizotolewa, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu aliweka bayana kwamba moja ya kuendelea kuwamo katika nafasi hizo kwa wakurugenzi hao ni utendaji kazi pamoja na ukusanyaji wa mapato ya ndani katika halmashauri.

Ni imani kwamba wale walioachwa katika 'mkeka' wa Rais ni wale walioonekana kutokufanya vizuri katika kilichopita na wale ambao walikuwa wakitoa lugha za maudhi dhidi ya wananchi pamoja na usimamizi mbovu wa rasilimali na ubadhirifu katika baadhi ya miradi ya maendeleo.

Viongozi hao walioteuliwa wana dhamana kubwa katika kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuwa ngazi hizo katika serikali ndilo chimbuko la kuibua mipango ya kuwaondoa wananchi katika umaskini na kuwaingiza katika neema. Kupitia serikali za mitaa, wananchi wana uwezo wa kubuni, kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kutokana na ukweli huo, wakurugenzi hao wana wajibu mkubwa kuhakikisha wananchi katika maeneo yao wanakuwa na ahueni ya maisha. Pia wana wajibu wa kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinatumika ipasavyo na matokeo chanya kuonekana.

Hata hivyo, katika miaka michache iliyopita, imeshuhudiwa baadhi ya wakurugenzi katika halmashauri wanakuwa na lugha chafu na wengine kujiona miungu watu. Wateule wapya wanapaswa kujifunza hilo na kuwa wanyenyekevu kwa kuwa wao ni watumishi wa wananchi na hawajapewa nafasi hizo kwa ajili ya kutumikiwa.


Kwa maneno mengine, wanatakiwa kujishusha badala yua kujikweza kama ilivyokuwa kwa wengine waliotangulia na wameachwa katika uteuzi mpya, hivyo watambue kwamba nafasi walizopata ni dhamana na si ufahari.

Tunawatakia kila la heri wateule hao na pia watambue kuwa wamepewa nafasi hizo si kwa hisani bali kutokana na kuaminiwa kuwa wana uwezo na sifa zinazostahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Haika Christopher, SJMC

# Ukikataa chanjo umependa corona

**SERIKALI** imezindua chanjo ya Johnson & Johnson's (Janssen), na kuanza kuchanja watu kujikinga na maradhi ya COVID-19 na kupunguza kusambaa kwa virusi vya corona nchini.

Ila pamoja na uzinduzi huo na viongozi wakuu kuchanjwa akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, bado baadhi ya watu wana mtazamo potofu kuhusu hatua hiyo.

Hilo limesababisha kuwahamasisha wengine wasichome chanjo kwa madai kuwa ina madhara kama damu kuganda, na wengine kusema kuwa watu watabadilika kuwa 'mazombi au mataahira' , na wengine kusema kuwa wanakufa mara baada tu yakupatiwa chanjo hiyo au hawatamaliza miaka miwili.

Pengine hakuna ushahidi kwamba baada ya kupata chanjo watu watakuwa wagonjwa kwani chanjo hazileti maradhi bali zinafundisha mfumo wa kinga ya mwili kutambua na kupambana na maambukizi ya vimelea au virusi vya ugonjwa ambao kwa wakati huu ni corona.

Baadhi ya nukuu za waliochanjwa kama Dk. Khamis Kigwangala, baada ya chanjo ya Johnson & Johnson's Janssen, anasema hajapata madhara si damu kuganda, homa wala kuchanganyikiwa.

Hata hivyo, Watanzania wana haki ya kujiuliza swali la msingi: Watu watafahamu vipi kuwa chanjo ni salama? Ni muhimu kutafuta jibu kwani hata wanasayansi walijiuliza wanapoanza kutengeneza chanjo mpya, na hivyo majaribio ya usalama wake huanza katika maabara, kwa majaribio na utafiti unaofanywa kwa seli na wanyama wadogo hadi wakubwa kabla ya kuhamishia majaribio hayo kwa binadamu.

Hivyo chanjo hii ingekuwa na madhara ni nani angejaribu kuchanja. Inawezekana yapo lakini si makubwa. Viongozi wamechanjwa ili kuonyesha kuwa ni salama. Kila mtu anao uamuzi wa kupatiwa chanjo hii ya corona ili kupunguza maafa yanayoweza kuzidi kujitokeza.

Pia kwa Watanzania walio na mtazamo potofu juu ya chanjo ya corona wangeacha kupotosha umma kuhusu madhara wanayoyasema, ni kwasababu hakuna utafiti wowote wa kisayansi ambao wameufanya hivyo wasipotoshe kwani uongo unasaidia kupunguza vifo nchini.

Kwa ushauri zaidi ningependa kuwahamasisha Watanzania kutokusikiliza wapotoshaji juu ya chanjo ya corona bali kusikiliza ushauri wa wana sayansi na madaktari maana hao ndiyo wanaoweza kuielezea dunia nini kifanyike na kipi kisifanyike ili kupatiwa chanjo ya corona kupitia utafiti na majaribio mbalimbali.

Hata hivyo, ni vyema kukumbuka kuwa chanjo ya corona ni hiari hakuna anayelazimishwa kuchanjwa lakini ninawahamasisha watu kwenda kupatiwa chanjo hii kwani wataalamu wanasema itapunguza idadi ya vifo nchini, maambukizi na kuongeza nguvu kazi hasa hasa kwa vijana wengi ili kuleta kwa pamoja uwezo wa kuongeza kipato na kuiinua uchumi wa nchi yetu.

Mamlaka mbalimbali zinaeleza jinsi uwekezaji wa Tanzania ulivyoathiriwa na corona, kama kituo cha uwekezaji (TIC) kinasema miradi ya uwekezaji imepungua kutokana na athari za virusi vya corona duniani, hatua ambayo imechangia uzorotaji wa ajira kwa Watanzania, hivyo ni jukumu la wananchi kupambana na janga hilo la corona kwa kukubali kupatiwa chanjo ili kuhakikisha uchumi na maendeleo yanasonga mbele, kurudisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali pamoja na utalii.

Watanzania wafahamu kuwa kupitia chanjo ya corona wanaweza kuongeza na kupandisha uchumi wa nchi kwa vile wataongeza afya ya nguvu kazi kwa kupunguza vifo, hofu na woga vitaondoka pia baada ya mili kuwa imara kupambana na magonjwa wakiendelea kuchapakazi ili kuchangia maendeleo ya taifa.

## HABARI KITAIFA

# RC awatoa hofu wananchi fidia

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (pichani), amesema wananchi wanaodai fidia katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Afrika Mashariki watalipwa kama ilivyokuwa katika tathmini ya awali iliyofanyika mwaka 2019.

Kunenge aliwatoa hofu wananchi hao katika kikao alichokifanya kwenye kijiji cha Manda Mazingara, Kata ya Mkange Halmashauri ya Chalinze ambacho alikiitisha baada ya kuwapo kwa malalamiko kwamba fidia zao zimepunguzwa.

Alisema wananchi wote watalipwa kwa kufuata vigezo vya tathmini ya awali kama walivyolipwa wananchi wengine wanaopitiwa na mradi huo katika maeneo ya Mkoa wa Tanga.

"Ninachowaomba mfanye subira tuacheni tukapambane na mtalipwa kwa utaratibu huo huo uliofanyika kwa wale wa upande wa Tanga kwa kuwa mradi ni mmoja sisi ni viongozi wenu mtuamini," alisisitiza.

Alisema katika tathmini ya awali kulitokea kikwazo cha fedha, hivyo kusababisha kuwa na mabadiliko ambayo hakutaka kuyaweka wazi kwa kuwa utaratibu mwingine unafanywa ili wananchi hao walipwe fidia zao,

"Serikali ya Rais Samia Sulluhu Hassani inawathamini wananchi wake, inawapenda, inafuata sheria na taratibu, hivyo utaratibu wa malipo utafanyika kama ilivyo kwa waliotangulia kulipwa kwenye mradi huu ambao ni wa mkoa jirani wa Tanga," alisema Kunenge

Alisema amechukua malalamiko hayo na ataenda kushauriana na wizara husika ili kupitia vigezo vilivyotumika kuwalipa wakazi wa Tanga vitumike pia na kwa Mkoa wa Pwani. Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah, alisema mradi huo wa ujenzi wa barabara ya Afrika Mashariki inayopita Bagamoyo, Saadani Makange, Mbweni, Pangani mkoani Tanga mchakato wake ulianza wakati wa serikali ya awamu ya nne na fedha za mradi huo zilikuwa zilipwe na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Andallah alisema ilipofika mwaka 2017 Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, baada ya kuona mradi unasuasua aliagiza zitengwe fedha za ndani Sh. bilioni 16 kwa ajili ya kuanza kujenga kilomita 50 kutoka Tanga hadi Pangani ujenzi ambao umekamilika.



Mkuu huyo wa wilaya alieleza kuwa baada ya kuona hali hiyo AfDB ilitenga Sh. bilioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 120 kuanzia Mbweni hadi Saadani.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Pwani, Mhandisi Andrea Kasamwa, alisema tathmini ya awali ilifanyika kwa mita 60 lakini baadaye ilipunguzwa na kufanyika kwa mara nyingine kwa mita 45 na kwamba upande wa Tanga waliolipwa fidia ni kwa mita 45.

Wananchi 421 wa kata ya Mkange ndio wanaodai fidia na kwamba kati yao ni wakazi wa Kijiji cha Manda Mazingara na wengine ni wa vijiji vya Gongo na Matipwili.

# Vibaka wavamia mawakala na kupora fedha Nachingwea

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wanaosadikiwa ni vibaka, wamevamia nyumbani kwa mawakala wa pesa katika Kata na Tarafa ya Naipanga, Nachingwea mkoani Lindi kisha kujeruhi na kupora simu na fedha taslimu zaidi ya Sh. 5,200,000.

Kwa mujibu wa baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo na kuthibitishwa na mamlaka husika ya ulinzi na usalama ngazi ya mkoa, uporaji huo umefanyika Ijumaa iliyopita saa 1:30 usiku.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, mashuhuda hao walisema jana kuwa watu wasiopungua sita wakiwa na nondo, walivamia nyumba wanayoishi mawakala wawili wa pesa na kutekeleza kile walichokikusudia.

Mashuhuda hao ambao hawakupenda kutajwa kwa majina yao, walisema baada ya kufika nyumbani hapo, walivunja mlango kwa kutumia jiwe kubwa, maarufu kwa jina la Fatuma, kisha kupora simu na fedha taslimu na kuondokana nazo.

"Baadhi ya vibaka walikuwa wamevaa soksi katika vichwa vyao zilizoachwa wazi sehemu za macho kwa lengo la kuficha sura zao," alisema mmoja wa mashuhuda hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwataja mawakala hao kuwa ni Omari Msavai (43) na Lauma Mohamed (23), wote ni wakazi wa Kata na Tarafa ya Naipanga.

Alisema vibaka hao wakiwa na nondo walifika kwenye nyumba wanayoishi mawakala hao na kuvunja mlango na kuingia ndani kisha kumjeruhi vidole viwili vya mkono wa kulia Msavai kwa kitu chenye ncha kali.

Kitinkwi alisema licha ya kujeruhi, vibaka hao walipora vocha zenye thamani ya Sh. milioni 1.5, simu mbili aina ya Infinix yenye laini 0625 163 982 na Nokia yenye laini 0657 480 600, zikiwa na fedha taslim Sh. milioni 5.2 na kuondoka nazo kusikojulikana.

Alisema tayari timu ya makachero imepelekwa kuendelea na kazi ya kuwatafuta vibaka waliohusika na uhalifu huo ili sheria ichukuwe mkondo wake.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

216387602

FSSP Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION FOR A GOVERNANCE SECTOR MAPPING SPECIALIST**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide individual consultancy Services as a Governance Sector Mapping Specialist to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The individual Governance Sector Mapping Specialist will provide technical support and advice to Global Affairs Canada through identifying opportunities for programming in the Inclusive Governance sector in Tanzania.

Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:

i. Master's degree in relevant discipline from a recognized University.
ii. Five (5) years of professional work experience in the international development sector in Tanzania.
iii. Five (5) years of professional experience in working with Development Partners.
iv. Five (5) years of professional work experience on governance, democracy, gender equality and human rights.
v. Previous experience in conducting similar scoping studies, preferably in the areas of inclusive governance, human rights and gender equality.
vi. Experience in working with stakeholders from Non-Government Organizations and Government

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

i. Strong report writing and oral and visual presentation skills;
ii. Knowledge of national context for governance in Tanzania, including an understanding of relevant policies, priorities and programs of key institutions and development partners.
iii. Advanced professional proficiency in spoken and written English – level 4 and Kiswahili – level 4 as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng**
iv. Knowledge of gender equality policy priorities and processes in Tanzania.

Interested individual candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **15th August 2021 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

216390701

# Gharama za nyaya zatajwa ni kikwazo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa kata za Buhembe, Nyanga na Nshambya katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wamesema baadhi yao wanashindwa kuunganisha umeme kwenye nyumba zao kutokana na gharama kubwa za kutandaza nyaya na kununua vifaa vingine.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema suala la kuandaa miundombinu ndani ya nyumba linachangia kukwamisha mtu kumudu gharama hizo.

Mmoja wa wananchi hao, Godfrey Ibrahim, alisema uhitaji wa kufungiwa umeme kwenye nyumba za watu ni mkubwa, lakini kikwazo ni gharama za kuunganishiwa huduma hiyo.

Alisema gharama za ukaguzi na kutandaza nyaya ndani ya nyumba na usogezaji wa nguzo za umeme kwenye makazi ni kikwazo kwa wengi.

Mkazi wa Kata Buhembe, Ayoub Haruna, alisema kushuka kwa gharama za kuunganisha umeme majumbani hadi kufikia Sh. 27,000 kumechangia watu wengi kutaka kuunganishiwa huduma hiyo lakini tatizo lipo kwenye gharama za kuweka miundomibu ya nyaya ndani ya nyumba.

"Nguzo za umeme zinawekwa mbali na makazi ya wananchi, hatua ambayo inasababisha watu wengi kushindwa kuunganisha umeme," alisema

Naibu Waziri wa Nishati, Steven Byabato, alisema taarifa za malalamiko ya wakazi hao kupunguziwa gharama za ukamilishaji umeme majumbani amezipokea.

Byabato alisema mbali na kupokea taarifa hizo, yapo pia madai kutoka kwa wakazi hao kwamba baadhi ya watumishi huingia mitaani na kuwaambia wananchi kwamba shirika halina vifaa vya kutosha.

"Nimepokea taarifa kuwa wapo baadhi ya watumishi wanaokwenda mitaani na kuwabia wateja wanaohitaji kufungiwa umeme," alisema Byabato.

Alisema serikali imeweka kiwango cha ufunga umeme ambacho kwa mijini na vijiji ni Sh. 27,000 kwa nchi nzima.

# Polisi wasaka silaha ya mkulima aliyeuawa

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi, linaendelea kutafuta silaha iliyokuwa ikitumiwa na mkulima wa Kijiji cha Nanjilinji 'B' Wilaya ya Kilwa, Chande Magoma, anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa fimbo kichwani na wafugaji kutoka Ruangwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, alisema hayo jana alipokuwa anazungumza na mwandishi wa habari hii ofisini kwake, mjini hapa.

Mauaji hayo yalifanyika Julai 20, mwaka huu, kutokana na kile kinachoelezwa mkulima huyo kuchukua uamuzi wa kufukuza mifugo iliyoingizwa shambani mwake ikilishwa mahindi yake.

Kitinkwi aliitaja aina ya bunduki hiyo kuwa ni Shotgun Greener Maker namba 36317 Calier 12, iliyokuwa inamilikiwa na Magoma.

Kitinkwi alisema Magoma alikuwa akimiliki bunduki hiyo kwa kitabu chenye namba ya umiliki 28257 ambayo baada ya kuuawa silaha hiyo pia ilitoweka na haijulikani iliko mpaka sasa.

Alisema suala la kutoweka kwa silaha hiyo si la mchezo kwa kuwa inapotoweka kwa mmiliki halali inaweza kutumiwa vibaya na mtu au watu wengine wenye nia mbaya kwa jamii.

"Wapo baadhi ya wanaoendesha vitendo viovu kama vile ujambazi, uporaji wa kutumia silaha lakini pia ujangili," alisema ACP Kitinkwi.

Alisema kwa kawaida silaha inapaswa iwe mikononi mwa aliyekabidhiwa kisheria na serikali ndiyo maana humpatia na kibali cha umiliki, hivyo Magoma alikabidhiwa kumiliki kwa kitabu namba 28257 kinathibitisha kumiliki bunduki iliyopotea katika vurugu za wafugaji na wakulima.

Baadhi ya mashuhuda katika kijiji cha Nanjilinji 'B', walisema Magoma aliuawa na wafugaji hao alipokuwa anawafukuza kutoka shambani mwake ng'ombe walioingizwa na wafugaji kulisha mazao yake.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha ushiriki wa maonyesho ya Biashara na Madini kwa Kaimu Meneja wa Benki ya Exim tawi la Shinyanga, Sarah Tito, yaliyohitimishwa mkoani Shinyanga hivi karibuni. Wengine ni Mkuu wa mkoa huo, Dk. Philemon Sengati (kushoto) na Mwenyekiti wa Tume ya Madini Tanzania Prof Idris Kikula (wa tatu kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yapongezwa kwa kujali wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, ameipongeza Kampuni ya SGA Security kwa rekodi yake maalum ya kuhakikisha wafanyakazi wake wanadumu kwa muda mrefu hadi umri wa kustaafu tofauti na kampuni zingine.

Ramadhan Kingai, akizungumza katika hafla maalum ya kuwaaga wastaafu 40 wa SGA akiwa mgeni rasmi, alisema kampuni hiyo inastahili kuigwa na kampuni zingine.

Kingai aliwapongeza wastaafu hao kwa kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuongeza kuwa walinzi wengi hushawishika kuingia katika ujambazi kutokana na vikwazo wanavyovipata kazini.

"Ninawaomba mkawe mabalozi wazuri wa amani katika jamii. SGA imedhihirisha kuwa inawajali wafanyakazi wake wanaobaki na wanaoondoka kwani mikataba ya kazi haionyeshi popote, kuwa mfanyakazi atapewa zawadi wakati wa kustaafu lakini SGA imeingia gharama hiyo, ni jambo la kupongezwa," alisifu.

Alitoa pongezi kwa uongozi wa kampuni hiyo kwa kuwa mfano pia katika kuhakikisha makato ya wafanyakazi yanawasilishwa kwa wakati na kuwahakikishia wafanyakazi kuhusu pensheni zao tofauti na kampuni zingine, ambazo zimekuwa na malalamiko mengi.

Kamanda huyo pia aliushukuru uongozi wa kampuni hiyo kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi, akipongeza kampuni kwa kuendelea kutoa huduma za viwango vya juu na kuendelea kulisaidia Jeshi la Polisi katika kuhakikisha kuna utulivu na wananchi wanafuata sheria. "Kampuni binafsi za ulinzi ni sehemu ya polisi jamii. Kuna amani na utulivu nchini, kwa sababu ya ushirikiano tunaopata kwenu," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu, alisema waanzilishi wa kampuni hiyo walihimiza nidhamu ya hali ya juu kwa uongozi kuhakikisha unayapa kipaumbele maslahi ya wafanyakazi.

Alisema hiyo ndio siri ya mafanikio ya kampuni hiyo.

SGA ndio kampuni kongwe binafsi ya ulinzi nchini iliyoanzishwa mwaka 1984, kipindi hicho ikijulikana kama Group 4 Security. Kwa sasa imeajiri wafanyakazi zaidi ya 5,000 nchi nzima.

Ndio kampuni pekee ya ulinzi yenye cheti cha ISO 18788 – Security Operations Management System. Mwaka huu kampuni hiyo ilipokea tuzo baada ya kutangazwa mshindi wa jumla kama kampuni yenye rasilimali za kutosha na ya kuaminika mwaka 2020 katika Tuzo za Chaguo la Wateja (Consumer Choice Award).

# Regency yaanza kutoa chanjo ya COVID-19

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Regency ya jijini Dar es Salaam, imeanza kutoa chanjo ya COVD-19 na wananchi mbalimbali wamekuwa wakimiminika kupata huduma hiyo.

Akizungumza jana hospitalini hapo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Lalit Kanabar, alisema wameanza kutoa chanjo inayotengenezwa na kampuni ya Johnson and Johnson ya Marekani.

Alisema wamepewa dozi hiyo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mganaga Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam na Wilaya ya Ilala ambapo watu wamekuwa wakijiandikisha kwenye tovuti ya https//chanjocovid.moh.og.

Kanabar alisema wananchi wanapojisajili kwenye tovuti hiyo wanapata usajili ambao unawezesha kwenda kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya kupata chanjo ambayo hutolewa bure.

Alisema hospitali hiyo itakuwa ikitoa chanjo hiyo kila siku hadi shughuli za utoaji wa huduma hiyo zitakapofikia mwisho.

Kwa mujibu wa Kanabar, huduma hiyo inatolewa bure wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi kupata chanjo hiyo na kuondoa hofu kwa kuwa haina madhara yoyote.

Mtu wa kwanza kupata chanjo hiyo hospitalini hapo, Hussein Athuman, aliwaondoa hofu watu wananoogopa akisema haina madhara kwa binadamu.

Alisema huduma hiyo imekuwa ikitolewa kwa haraka na wala mtu anayetaka hawezi kukaa foleni kutokana na utaratibu mzuri ambao umeandaliwa sehemu hiyo.

# Serikali kupeleka chanjo ya corona kambi za wakimbizi

**Na Abubakari Akida,** MOHA

SERIKALI imesema iko katika mpango wa kupeleka chanjo ya Uviko-19 katika kambi na makazi ya wakimbizi mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi ili kukabiliana na wimbi la tatu la ugonjwa huo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, wakati alipotembelea Kituo cha Afya cha Katumba kinachotumiwa na wakimbizi na raia wapya wanaokadiriwa kufikia 86,233 toka nchini Burundi ambao walikimbia mapigano ya kikabila yaliyotokea nchini kwao 1974.

"Katika kukabiliana na janga la Uviko-19 tayari wakuu wa makambi wameshaanza kutambua idadi ya watu ambao wanauhitaji wa hiari wa kupata chanjo hiyo," alisema Chilo.

Akizungumzia idadi ya wagonjwa wa Uviko-19 katika kituo hicho cha afya, Mganga Mfawidhi, Dk. Veneranda Msati, alisema hawana mgonjwa aliyefika kituoni na kwamba elimu ya kujikinga na ugonjwa huo inatolewa kwa wagonjwa na wajawazito wanaofika katika kituo hicho kupata huduma.

"Kwasasa katika kituo chetu hatuna mgonjwa yeyote wa corona tunachofanya ni kutoa ushauri wa kujikinga na maradhi hayo kwa wagonjwa wanaofika hapa kupata huduma za afya ikiwamo wajawazito," alisema Dk. Veneranda.

Awali, akisoma taarifa ya makazi hayo, Mkuu wa Makazi ya Katumba, John Mwita, alisema hali ya usalama ni shwari huku wakiendelea kutoa elimu na kufuata sheria za kuishi katika makazi kwa wakimbizi hao.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Masauni (katikati), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania (UTT AMIS), Simon Migangala (aliyenyanyua mikono), wakati alipotembelea taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 1.59/- kujenga barabara Bumbuli

**Na Thobias Mwanakatwe,** LUSHOTO

SERIKALI imelipatia Jimbo la Bumbuli, wilayani Lushoto mkoani Tanga Sh. bilioni 1.59 kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami na changarawe.

Mbunge wa Bumbuli, January Makamba, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mponde katika mfululizo wa ziara yake ya kukagua na kuweka mawe ya msingi miradi mbalimbali inayotekelezwa katika jimbo hilo.

Aliwaambia wananchi atahakikisha anapigania na kulipeleka bungeni suala la changamoto ya barabara lililopo maeneo ya vijijini ili kuwapo usawa kati ya mjini na vijijini.

Alisema fedha zilizotolewa na serikali zitatumika kujengwa kwa kiwango cha changarawe barabara ya Mgwashi - Mbelei yenye urefu wa kilometa 23.8, Bumbuli -Mayo, Vulii- Mahezangulu hadi Magoma kilometa 15.4, Vuga - Mponde hadi Wena kilometa 21.2 na Balangai - Tamota na Vuliii yenye urefu wa kilometa 13.4, Soni -Mponde kilometa 13.4 pamoja na Bumbuli center itakayojengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema sio sawa kuona mjini wanajengewa barabara za juu na zinapanuliwa kila kukicha, lakini vijiji ambako kuna wapigakura wengi wanapata shida kupitisha mazao yao kutokana na barabara hasa wakati wa msimu wa mvua.

"Mimi huwa nawaambia wenzangu kama kweli tunaweka barabara za maghorofa hatushindwi kuwasaidia watu wa vijijini kwani wanachotaka barabara zao zipitike wakati wote hasa kipindi cha mvua," alisema.

Alisisitiza lazima kuwapo na haki sawa katika kupeleka maendeleo ya nchi.

Alieleza kuwa moja ya malengo makubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Hassan Sulluhu ni kupambana na barabara za vijijini.

Pia serikali imepanga ifikapo mwaka 2025 Watanzania wanaokipigia Chama Cha Mapinduzi kila mwaka, angalau barabara zao ziwe zinapitika wakati wote sababu hao tunaowajengea za maghorofa yawezekana baadhi yao hawapigi kura wakati wa uchaguzi.

Alisema kiu yake ni kuona wananchi wake wanaondokana na changamoto hiyo ambayo ni kero kubwa ya maeneo ya Jimbo la Bumbuli.

# DC atinga stendi ili kukagua utekelezaji kujikinga corona

**NA Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, amefanya ziara ya kushtukiza saa 11:00 alfajiri katika Stendi Kuu ya mabasi ya kwenda mikoani na vijijini iliyoko Igumbilo kwa lengola kukagua utekelezaji wa kitaifa wa kupambana na corona.

Kiongozi huyo alifanya hivyo juzi kujiridhisha kama wananchi wanachukua tahadhari kwa kunawa mikono, kuvaa barakoa na abiria kukaa kwenye viti na hakuna anayesimama.

Alisema alifanya ziara hiyo kukagua mabasi yote yaendayo mikoani kama abiria wamechukua tahadhari ilivyoagizwa na serikali.

Moyo alisema maagizo hayo ya kitaifa yanapaswa kutekelezwa kwa vitendo kwa kuhakikisha wahudumu wa mabasi ya kwenda mikoani na wanachukua tahadhari kama ilivyoelekezwa.

Kwa mujibu wa Moyo baadhi ya abiria walikuwa hawatekelezi maagizo hivyo kutoa amri kuwa ni lazima kila mmoja hana budi kuchukua hatua.

Licha ya abiria na wahudumu wa mabasi, alisema wananchi pia popote walipo katika Wilaya ya Iringa, hawana budi kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kutumiavitakasa mikono na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni na kuepuka na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Katika hatua nyingine, Moyo alisema hivi sasa Tanzania Bara na Zanzibar chanjo ya corona imefika, hivyo wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi kupata chanjo hiyo. Aliwaomba wananchi kujitokeza ili kuwaunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi wa Zanzibar kupata chanjo hiyo kwa kuwa haina madhara yoyote kama baadhi ya watu wanavyotangaza.

Baadhi ya wananchi na wakazi wa Manispaa ya Iringa wakiwamo Charles Mhilu na Rehema Said, kwa nyakati tofauti walimpongeza mkuu wa wilaya kwa kutoa elimu juu ya kijikinga na corona wakati wa ziara zake.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania, Charles Itembe (wapili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga (kulia), wakibadilishana hati za mkataba, Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano yatakayowawezesha wakulima wa mazao ya kimkakati kupata bima ya afya kwa njia ya mkopo usio na riba, utakaotolewa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawatoa hofu wakulima kuhusu mbolea

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewahakikishia wakulima kuwa mapema mwezi huu shehena ya mbolea yenye zaidi ya tani 60,000 itaingia nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo, alisema juzi kuwa kati hizo tani 38,000 ni mbolea ya aina ya CAN ambayo itaingia kati ya Agosti 10 na 12.

Pia alisema tani 33,000 ni UREA ambazo zitaingia nchini kabla ya mwishoni mwa mwezi. Pia alisema tani 16 zingine za aina ya UREA zitaingia baadaye.

"Kwa hiyo ukijumlisha hapo kuna kama tani za UREA 50,000. Hiki ni kiasi kingi cha mbolea na kimsingi mbolea nyingi itaingia zaidi kwa hiyo niwatoe hofu wakulima kwamba mbolea itakuwapo," alisema Ngailo.

"Na kwa habari ya bei serikali inaangalia namna ya kupunguza makali. Kwa hiyo serikali haijalala inafanya kazi kuhakikisha kwamba mkulima anapata mbolea kwa wakati na kwa bei ambayo anaweza akaimudu," alisema.

Ngailo pia alisema kwa mikoa ya Iringa, Ruvuma na Njombe suala la upatikanaji mbolea linaridhisha kwa kuwa ina takribani tani 8000.

"Iringa kuna zaidi ya tani 1,000, Ruvuma kuna zaidi ya tani 2,000 na hapa Njombe kuna zaidi ya tani 5,000 na hii tunasema si msimu hasa kwa hiyo tuna uhakika kwamba mbolea itaendelea kuingia katika mikoa hii na upatikanaji wake hautakuwa na shida," aliongeza.

Ili kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo, mkurugenzi huyo alihimiza Watanzania kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya mbolea.

Naye Meneja Mkuu wa Mtewele General Traders, Sady Mwang'onda, aliwatoa hofu wakulima kuwa maghala yao yana pembejeo za kutosha na kwamba kuna mbolea nyingine iko njiani.

"Tunajiandaa na msimu wa kilimo. Tuna magari mengi yanaleta mbolea kutoka Dar es Salaam kuja hapa na kwa kadiri msimu unavyozidi kusogea na sisi tutaendelea kuleta mbolea ya kutosha ili kuhakikisha mkulima hapati shida ya kuipata," alisema.

# Benki yaadhimisha miaka 5 ya falsafa ya 'Mteja Kwanza'

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya UBA imeadhimisha miaka mitano ya falsafa yake iitwayo 'Mteja Kwanza'.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa UBA, Kingsley Ulinfun, ilisema kuwa falsafa hiyo ilizinduliwa mwaka 2016 ikiwa na lengo la kuifanya benki kuwa na mwelekeo na mtazamo kwa wateja.

"Hii ikibeba maana kubwa sana ya kuwaelewa wateja na kuwaweka mbele na kuwachukulia kwa uzito mkubwa mahitaji yao hasa katika kila tunachofanya katika huduma zetu za kila siku," alisema.

Alifafanua kwamba falsafa hiyo pia inatumika katika bidhaa na huduma bunifu zilizoboreshwa, zinazotolewa na UBA ambazo hulenga katika kumwezesha mteja afaidike na kumuinua kimaisha.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na kukua na kuongezeko kwa miamala ya kielektroniki, UBA imetengeneza kituo ili kufuatilia kwa ukaribu malipo na miamala mingi hivyo kuweza kuboresha kwa kiasi kikubwa huduma kwa wateja.

"Pia wateja wamepewa fursa ya kuweza kuperuzi akaunti zao popote na kwa wakati wowote wakitumia huduma bora kabisa za Benki ya UBA. Huduma hii pia inapatikana kupitia simu janja, kompyuta, kompyuta mpakato na vifaa vingine vyote vinavyoweza kutumia huduma ya mtandao," ilisema taarifa hiyo.

Pia ilisema UBA inatarajia kutengeneza majibu na maazimio juu ya malalamiko ya wateja, usimamizi wa uhusiano bora kati ya viongozi na wateja, mawasiliano makini na salama kwa wateja juu ya bidhaa na huduma za benki.

**"Hii ikibeba maana kubwa sana ya kuwaelewa wateja na kuwaweka mbele na kuwachukulia kwa uzito mkubwa mahitaji yao hasa katika kila tunachofanya katika huduma zetu za kila siku," alisema.**

## MJADALA WA KATIBA MPYA
### Hoja ijikite kwenye taifa kuunda taasisi imara

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## FILIPE JACINTO NYUSI
### Rais wa Msumbiji anayetishiwa hatima na waasi

siasa

JUMATANO AGOSTI 4, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

SINTOFAHAMU CHANJO CORONA

# Wataalamu, wanasiasa wameikubali ni zamu ya raia kuondoa kigugumizi

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

WAKATI wanasiasa na wataalamu wanakubaliana kutumika chanjo ya corona , na wengine wakitaka iwe lazima na si hiyari kuchanja, bado wananchi wanabaki kwenye sintofahamu kuhusu kupokea chanjo hiyo.

Hayo yanajiri baada ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akiwa mjini Mwanza mwezi uliopita kabla ya kukamatwa na kufunguliwa mashtaka, alisisitiza umuhimu wa chanjo ya COVID-19 kwa Watanzania, akitaka serikali iifanye kuwa suala la lazima na sio hiyari.

Anapinga maelekezo kuwa chanjo ni hiyari kwa akatayependa, akieleza kuwa Shirika la Afya Duniani (WHO) linaelekeza kuwa ni lazima.

Mbowe anakumbusha kuwa matibabu ya mgonjwa wa COVID-19 anapolazwa yanagharimu zaidi ya Shilingi milioni 10 kwa wiki mbili, akitoa ushuhuda wa kuuguza ndugu zake, ambao kwa siku mmoja alitumia mitungi minne na kila mmoja ukitozwa Shilingi 30,000, akihoji ni wangapi wanaweza kulipa gharama hizo ?

Licha ya matibabu hayo kupaswa kubebwa na serikali, bado ni mzigo mkubwa, hivyo ni vyema kupunguza maambukizi kwa kutoa chanjo kwa kila mmoja kwa lazima.

Wakati hayo yakijiri kampeni za kuchanja zinakutana na vigingi vya kuipinga serikali kukubali chanjo ya Johnson Johnson , wengine wakitumia nguvu nyingi kusisitiza kuwa ukichanja umekwisha wakiaminisha wenzao kuwa kula malimao, tangawizi, kivumbasi na kupiga nyungu kunaweza kupambana na corona.

Hata hivyo, ukweli unabaki pale pale kuwa corona ni suala la dunia nzima, Rais Samia Suluhu Hassan, kama anavyosema taifa haliwezi kukimbia chanjo japo anawaeleza Watanzania kuwa ni hiyari, lakini anahoji nchi ingewezaje kukaa kimya wakati dunia nzima inazungumzia chanjo, ili kukabili maradhi hayo na kupunguza kasi na wingi wa maambukizi?

Mapema mwaka huu taarifa za Shirika la Afya Duniani WHO, ziliitaja Tanzania, Chad, Burkina Faso, Burundi, Eritrea na Madagascar kuwa zilikuwa zimekomaa na kukataa chanjo kwa maelezo kuwa mataifa hayo hayana maambukizi ya corona, tena yana tiba za asili na kuwahimiza watu kuendelea na tiba zinazozalishwa na wataalamu wa mataifa hayo.

WHO inasema Madagascar imeanza kuchanja watu wake, aidha Juni Chadi ilianza kutoa chanjo wakati Burkinafaso kama Tanzania imeanza kuwachanja wananchi wake mwezi uliopita. Hali ilivyo leo Afrika nzima imeanza kuchanja hivi Tanzania ingekuwa kisiwa kuendelea kukataa kuwa hakuna corona na kama inatokea watu waendelee kupiga nyungu, kula tangawizi na malimao? Pengine hilo lingehitaji mjadala zaidi, lakini kama Rais anavyosema dunia nzima inapambana na maradhi hayo, asingeweza kukaa kimya ndiyo sababu akaunda timu ya wataalamu kuishauri serikali kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya corana na chanjo ni mojawapo wa kile wataalamu walichopendekeza.



Freeman Mbowe ni miongoni mwa wanasiasa wanaotaka chanjo iwe lazima na alitangaza kuwa amechanjwa chanjo ya AstraZeneca. **PICHA: MAKTABA.**

Korea ya Kaskazini kwa mujibu wa Shirika la Habari la BBC ni taifa lililokuwa linapinga matumizi ya chanjo ya COVID-19 lakini hata hivyo limepokea dozi kutoka Russia za chanjo iitwayo 'Sputnik V' na kwamba taifa hilo muda wote lilikataa kuwapo kwa maradhi ya corona na kupinga chanjo kutoka mataifa mengi na kuikubalia Russia pekee, hata Rais wake Kim Jong-un hajakubali kuchanja.

**KUZALISHA CORONA**

Hivi Watanzania wangependa taifa libaki pekee duniani bila kupambana na maradhi hayo yanayoangamiza watu kwa kasi? Kukataa chanjo inamaanisha kukubali kufa kwa COVID-19 , pengine kutengwa na dunia, majirani kama wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na jumuiya ya wataalamu kwa vile taifa lingeonekana kama halikubaliani na teknolojia wala sayansi za tiba.

Tanzania na Madagascar zilieleza msimamo wake kuwa haziko tayari kuwa sehemu ya mpango wa kimataifa wa mgawanyo wa chanjo (COVAX) unaosimamiwa na WHO, licha ya mataifa kama Burundi na Eritrea kueleza nia ya kujipanga na kujiunga.

Wengi watakumbuka kuwa mwaka jana serikali ya Madagascar ilikaririwa ikisema kuwa haitashiriki kwenye mpango wa COVAX na itaendelea kutumia dawa yake ya miti iliyogunduliwa na wataalamu wa taifa hilo ikiwa ni vidonge pamoja na dawa ya maji ambayo Tanzania iliiagiza ili kufanyiwa majaribio na utafiti zaidi kwenye taasisi ya utafiti wa tiba za (NIMRI).

Kwa ujumla kuendeleza imani kuwa chanjo ni hatari au wanaochanja watakufa baada ya miaka miwili au mitano, ama watapungukiwa nguvu za kiume, watakuwa tasa na wameharibu mifumo ya nasaba (DNA) kwenye miili yao, wajiulize hivi wanapenda kuona taifa likibakia kuwa mazalia ya virusi vya corona?

Tanzania 'iheshimike' kama eneo la kuzalisha corona kwa sababu mataifa jirani na bara la Afrika kote wamechanja. Ni wazi ingesalia kuwa na wagonjwa kila mara, kupoteza maisha ya nguvukazi, kuzalisha virusi hivyo ambavyo pia vingekuwa vinatoa vizazi vipya (mutations) lakini pia kuendelea kuwa kisiwa cha wasiotumia sayansi na teknolojia katika tiba.

Hivi karibuni Waziri wa Afya Dk. Dorothy Gwajima, ameeleza hali ilivyo nchini akisema wapo wagonjwa zaidi ya 682 wengi wanatumia gesi au wanapumulia mashine na baadhi ya mikoa ambayo ina hali mbaya ni pamoja na Kilimanjaro, ambao wameanza kuchanja wiki hii.

Ukweli ni kwamba watu wanakufa na mitungi ya gesi haitoshi, na kwa mujibu wa taarifa za Hospitali ya KCMC, mkoani humo, mgonjwa anatumia kati ya mitungi 10 hadi 12 kwa siku na hospitali hiyo ina uwezo wa kuzalisha mitungi ya gesi 400 kwa saa 24 .

Inaongeza kuwa idadi ya wagonjwa wanaopokelewa ni 400 kwa siku na haina uwezo wa kuwahudumia kutokana na mahitaji makubwa ya gesi kusaidia kupu-

INAENDELEA UK. 12

# Serikali iuangalie ushauri huu wa Askofu Bagonza



'Mtumishi wa Mungu' Askofu Benson Bagonza, anasisitiza umuhimu wa kuwapo uvumilivu wa kisiasa. **PICHA: MTANDAO.**

**NA Mwandishi Wetu**

ASKOFU Benson Bagonza wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, ni miongoni mwa viongozi wa dini, wanaoamini kuwa jukumu lao ni pamoja na kulea waamini lakini pia kushauri jamii pamoja na serikali na wadau wengine ili kujenga taifa lenye uthabiti kisiasa, kiuchumi na kufikia maendeleo .

Wiki hii Askofu Bagonza, anazungumza na gazeti hili kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa na kijamii ambayo anaishauri serikali na wadau wengine kuyatupia macho ili kuwa na Tanzania inayompa nafasi kila mmoja kuishi kwa furaha.

Anaanza na kuzungumzia hali ya kisiasa nchini akisema inahitaji kuwapa furaha Watanzania kwa sababu, matumaini ya watu wengi baada ya mabadiliko ya serikali yameshuka.

Anafafanua kuwa kwa vile Watanzania huishi kwa matumaini si kwa vitu halisi, matumaini wanayojiwekea yakishuka wanakuwa na mashaka zaidi.

Akizunguma na Nipashe kuhusu mtizamo wake wa hali ya kisiasa nchini, anasema kwa sasa mashaka ni mengi kuliko matumaini.

Anaongeza kuwa kiwango cha uvumilivu wa kisiasa ni kidogo na kukumbusha kuwa kilitoweka katika awamu iliyopita, kikaanza kukua tena katika awamu hii.

> "Ghafla kimezimika kama mshumaa kwenye upepo mkali. Kuna watu wananufaika kiuchumi katika mradi wa kukosa uvumilivu wa kisasa." Anaonya Mtumishi wa Mungu, Bagonza.

"Ghafla kimezimika kama mshumaa kwenye upepo mkali. Kuna watu wananufaika kiuchumi katika mradi wa kukosa uvumilivu wa kisasa." Anaonya Mtumishi wa Mungu, Bagonza.

Akizungumzia kuwapo mjadala wa kitaifa baina ya Serikali na Vyama vya Upinzani, anaunga mkono kuwepo mazungumzo hayo na kuonya kuwa asiyetaka kuzungumza hataki amani.

"Anayetaka vita hapendi mazungumzo, hakuna katikati. Kuna vita vinavyoanzishwa na mazungumzo lakini pia humalizwa kwa kuzungumza. Wanaokwepa mazungumzo ni suala la muda tu. Meza hiyo haikwepeki. Ni ama uikatae au ujue kuwa utaikimbilia baadaye. Hakuna aliyewahi kushindwa kwa kutumia mazungumzo. Meza na kitanda ni viwanja vya kutunza amani katika jamii." Anakumbusha.

**KUWAPO SINTOFAHAMU**

Anapoulizwa iwapo mambo bado hayatabiriki kwenye ulingo wa kisiasa anakiri kuwa kuna sintofahamu suala la mikutano ya upinzani halijakaa sawa wala katiba mpya haijafahamika hatima yake.

Anasema katika vyombo vingi mfano bungeni hasa suala la wabunge wa viti maalumu wa CHADEMA bado ni sintofahamu.

Lakini pia vyombo vya usalama na polisi dhidi kambi ya upinzani kuna ukungu, akieleza kuwa sababu ni serikali kushindwa kuponya vidonda vya "hulka mpasuko" (polarization) vilivyorithiwa kutoka awamu iliyopita.

Anasema jambo hilo limegeuka kuwa suala mwendelezo wa kutoka awamu ya tano na kusema kinachotakiwa sasa ni kuweka wazi kuwa wataongoza nchi "kimpasukopasuko" ili Watanzania wazoee.

**ANAPENDEKEZA UFUMBUZI**

Askofu Bagonza anashauri umuhimu wa kuizungumzia serikali kuhusu kuwapo mpasuko, ili iukubali na viongozi wabadilike.

" Ziko dalili kuwa hawajui wanakwenda wapi? Na asiyejua aendako hapotei njia. Natamani serikali ingeanza upya kwa kusuka safu mpya na kuzungumzia maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwani ni wazi wapo viongozi wengi wanaojaribu kuyafahamu maono ya Mama kupitia hotuba zake katika matukio lakini bado hawayaelewi. "

Anamshauri Rais kukaa pamoja nao na kuwauzia maono yake ili wayafanyie kazi na kwamba jumuiko hilo ni muhimu kwa vile hii ni serikali na bunge la chama kimoja ambayo inaweza kukosa watu wa kuikosoa.

**KUTOWADHAMINI WANAOKAMATWA**

Akizungumzia msimamo wa CHADEMA kutowadhamini wanachama wake wanaokamatwa na polisi, anaiita hali hiyo hatua mpya inayoashiria makubwa mbeleni.

Anaongeza: "Wazo la kuua na kujiua huanzia kichwani. Vitendo hufuata baadaye. Kwa nini mtu akatae kudhaminiwa? Wanahitajika washauri nasaha wa kuwasaidia wanaokamata na wanaokamatwa."

Anasema zaidi sana anajiuliza, kudai katiba mpya ni kosa la jinai? Kama si kosa, anasema naye anaunga mkono wasidhaminiwe kwa sababu kumdhamini mtu asiye na kosa ni kosa pia.

"Kama mtu anatekeleza takwa la kisheria na kikatiba, anayemkamata ndiye anahitaji dhamana kwa kukiuka katiba." Anaongeza Askofu Bagonza.

**WITO KWA SERIKALI**

Askofu Bangonza anaikumbusha serikali kuhusu kuwapo amani, uvumilivu na uhimilivu wa kisiasa na kuishauri serikali na vyombo vyake kuacha kuchokoza wananchi.

Anafananisha kuwa hata kama mtu anawadharau siafu kuwa ni wadudu wadogo, hawezi kuwakalia kwa bila kuwa na mavazi ya kujikinga.

Anaeleza kuwa historia inaonyesha kuwa wananchi wakichoka wanaweza kukosa uvumilivu hivyo ni vyema kusikiliza kila upande, kutenda kwa haki na wakati wote kukumbuka kuwa taifa ni watu na ndiyo nguvu ya serikali.

## WATAALAMU, WANASIASA WAMEIKUBALI NI ZAMU YA RAIA KUONDOA KIGUGUMIZI

**INATOKA UK. 11**

mua na wodi za kuwahudumia.

Je, bado watu hawajaona umuhimu wa chanjo? Watanzania wangejaribu kufikiria iwapo zitakosekana wodi za kulaza wagonjwa, itakosekana pia mitungi ya gesi kusaidia wanaoshindwa kupumua, vyumba vya kuhifadhi miili ya wanaokufa kwa COVID-19 kujaa na ikakosekana sehemu ya kuhifadhi na watu wengi kuzikwa kila siku mijini na vijijini hali itakuwaje?

Lakini, si hivyo tu, Tanzania itakuwa peke yake ikihangaika na corona, kuibuka virusi vipya na wimbi moja baada ya jingine, kwa sababu huenda mataifa jirani na dunia ingeifungia mipaka na kuiwekea vikwazo vya kibiashara, kidiplomasia na kusingekuwa na dawa wala vifaa tiba, wala ushirikiano na taasisi za kimataifa za tiba kama WHO na COVAX. Hili nalo watu wangependa kuliona?

**KAMPENI KUBWA KUCHANJA**


Wakati chanjo zinaendelea kujadiliwa kwenye mitandao ya kijamii, makundi ya vijiweni ndani ya familia na kwingineko suala la msingi ni serikali na wadau kutumia nguvu ile ile ya kusema kuwa Tanzania haina corona kuhamasisha watu kuchanjwa kwa sababu corona ipo na inatisha.

Lengo ni watu kubadilika na kuachana na fikra za kizamani kuwa Tanzania haihitaji chanjo

Itakumbukwa awamu ya tano ilisema hakuna corona na kwamba wale wanaoumwa watumie nyungu, tangawizi na malimao pia taifa limuombe Mungu.

Juhudi hizo sasa zielekezwe kwenye kuhamasisha watu kuchanja, kuongeza kinga kwa kula malimao na tangawizi, kuongeza joto kwa kupinga nyungu na kumuomba lakini pia kuchukua tahadhari zote kama kuvaa barakoa, kukaa mbalimbali na kunawa mikono na kukwepa mikusanyiko.

Kampeni hizo zilenge mikoa 10 ya kipaumbele kuhimiza watu kujisajili ili kuchanjwa maeneo yalitangazwa kwenye mikoa ya Singida, Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Kigoma , Dodoma , Iringa na Mtwara ambako hali ni mbaya.



Abbas Mwalimu, mchambuzi wa siasa. **PICHA: MTANDAO**

MJADALA WA KATIBA MPYA

# Hoja ijikite kwenye taifa kuunda taasisi imara

**Na Sabato Kasika**

MAMBO yanayoteka mijadala na kuwa na nafasi kubwa katika mitandao ya kijamii wakati huu ni mazungumzo yanayohusu chanjo ya COVID-19 bila kusahau, suala la katiba mpya ambalo halijawekwa kando.

Licha ya kuwapo chanjo ya Johnson & Johnson au Janssen inayotolewa nchini na kuendelea kujadiliwa, itakumbukwa kasi ya kujadili katiba mpya imeendelea kuongezeka baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuomba wananchi, hasa wanaodai andiko hilo, kumpa muda ili aimarishe kwanza uchumi.

Akizungumzia katiba, mchambuzi wa siasa ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Kurasani Dar es Salaam, Abbas Mwalimu, anasema, hoja ya katiba ianze kujikita zaidi kwenye taifa kuwa na taasisi imara.

"Ili tuweze kupata upana wa hoja, ni vema kwanza tupambanue taasisi imara ni zipi? Je, zinatokana na katiba? Je katiba iliyopo haileti uwezekano wa kujenga taasisi imara? Ni muhimu kujadili hayo," anasema Mwalimu.

Anazitaja taasisi hizo kuwa ni zile zinazowawezesha wananchi kufanya kazi kwa ushirikiano na kwa amani, kutoa haki kwa wote kwa kuzingatia usawa, na kwamba zinaweza kuwa za kiserikali au za binafsi.

"Taasisi imara inatazamwa katika maeneo tisa ambayo ni ujumuishi, uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria, kupambana na rushwa, kutoa haki, usimamizi wa amani, kutoa huduma za msingi na umiliki," anasema Mwalimu.

Kwa maelezo yake, kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kutaka apewe muda aimarishe uchumi kwanza, inazingatia hoja ya kuwa na taasisi imara ambayo inataka serikali ijenge miundombinu wezeshi ya kiuchumi.

"Ujenzi wa barabara, reli ya kisasa ya umeme (SGR), bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, ununuzi wa meli, ujenzi wa bandari, hospitali, vifaa vya tiba, kujenga za sayansi na nyinginezo, utoaji wa elimu msingi bure na huduma ya afya ni kipaumbele," anasema.

Anahoji kuwa hata kama serikali ikikubali katiba mpya, ikiwa rushwa imetamalaki na kujitokeza kwa migogoro kama ilivyo kwa baadhi za nchi za Kiafrika Watanzania watakuwa wamekidhi hoja ya taasisi imara?

**MIFANO ILIYOPO**

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, hoja hiyo ya taasisi imara kabla ya katiba mpya inabebwa na mifano hai ya nchi kama Kenya ambayo wakati ilipopitisha mabadiliko ya katiba yao miaka kadhaa iliyopita ilionekana kuwa imefaulu.

"Sote tulisema na kuisifu kuwa ni mfano wa katiba bora katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki, lakini tujiulize, bila ya busara za Rais Uhuru Kenyatta baada ya Januari 30, 2018 Kenya isingekuwa imetapakaa damu?"

"Raila Odinga wa Muungano wa CORD, alijiapisha au aliapishwa pasipo uhalali kuwa Rais wa Kenya, lakini Kenyatta hakujali hili," anasema.

Anakumbusha kuwa ingawa alijiita rais wa watu, lakini Katiba ya Kenya kama zilivyo za nchi nyingi duniani zinasema 'kutakuwa na rais mmoja tu'. Hivyo, kwa kitendo kile cha 'kujiapisha' na kwamba kama Rais Uhuru ambaye wakati ule alikuwa Addis Ababa kwenye Mkutano wa Umoja wa Afrika asingemuamuru waziri wake wa usalama wa raia aondoe askari pale Uhuru Park huenda nchi hiyo ingekuwa katika machafuko makubwa.

"Lakini tujiulize pia, licha ya Kenya kuwa na katiba inayoelezwa kuwa ni nzuri, rushwa ipo kwa kiasi gani? Ikoje hali ya mafukara na matajiri? Je, Kenya ina taasisi imara ikiwa mara kwa mara inakutana na changamoto ya kupungukiwa na chakula kiasi cha kuagiza kutoka Tanzania?

Anasema, Afrika ya Kusini inaelezwa kuwa na katiba bora zaidi katika ukanda wa Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) lakini mbona haijawa na tija kwani inaelezwa kuwa umaskini ni mkubwa mno nchini humo.

"Ni kwa kiasi gani kuna amani Afrika ya Kusini? Ni kwa nini kumekuwa na wimbi la chuki dhidi ya weusi mara kwa mara? Taifa hilo lina taasisi imara licha ya kuwa na katiba bora?" anahoji .

**NINI KIFANYIKE?**

Mwalimu anasema, ni muhimu kujenga tabia ya uwajibikaji na kwamba hilo linafaa kupigiwa debe na watu wote, huku kuwajibika huko kukianzia kwa mtu binafsi, kuhimiza utamaduni huo kitaasisi na lisiwe jambo la sekta za umma au serikali pekee bali hata sekta binafsi.

"Rais wetu ameonyesha wazi kuwa anataka kujenga hilo pale alipowaomba wabunge waikosoe serikali na kuielekeza inapokosea bila kupepesa macho, lakini pia alieleza hayo alipokutana na wahariri wa vyombo vya habari," anasema.

Rais anaeleza wazi kuwa hakatai serikali yake kukosolewa bali anayekosoa atoe na njia mbadala wa kile alichokiona kina walakini na pia ukosoaji uzingatie adabu na heshima ya Kiafrika.

"Hapa tunaona Rais anataka kutujengea tabia ya kushiriki katika uamuzi na kuhoji mambo sambamba na kutoa ufumbuzi, akitazama dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika ujenzi wa taasisi imara," anasema.

Anafafanua kuwa ni muhimu kujikita zaidi kutengeneza taasisi imara, lakini pia kuwaelimisha wananchi kuifahamu katiba ya nchi, kwa kuwa ni wachache wanaojua haki na wajibu wao ulioainishwa kikatiba.

"Tusipojenga hoja thabiti katika haya maeneo ya taasisi imara, ikitokea tukapata katiba mpya huko baadaye, kama hakuna misingi bora kwenye mijadala ya kuwa na taasisi imara tutakuwa tumejidanganya," anasema Mwalimu.

> "Wananchi wanatakiwa kuhoji taarifa za mapato na matumizi ya kata au halmashauri zao, kuhoji wabunge wao waliowachagua ili wapate taarifa za fedha za mifuko ya jimbo," anashauri mchambuzi huyo.

Anasema, masuala ya uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji, lakini pia wananchi kuhoji yale ambayo yameahidiwa na wabunge, madiwani na wenyeviti wa serikali za mitaa au serikali ni muhimu.

"Wananchi wanatakiwa kuhoji taarifa za mapato na matumizi ya kata au halmashauri zao, kuhoji wabunge wao waliowachagua ili wapate taarifa za fedha za mifuko ya jimbo," anashauri mchambuzi huyo.

Anaongeza kuwa baadhi ya wananchi hawajui umuhimu huo na hawashiriki katika uamuzi wa masuala ya kisera unaohusu mustakabali wao na hata kipindi cha kampeni hawafanyi hivyo.

"Kama watu wanahoji wawakilishi wao bila kupata mrejesho, hapo kuna tatizo kwenye dhana nzima ya taasisi imara," anasema.

Mchambuzi huyo wa siasa anafafanua kuwa, iwapo wananchi hawawahoji lolote wawakilishi wao, lakini wanadai kuwapo kwa katiba mpya, basi wenyewe (wananchi) ndiyo wenye tatizo.

## JUKWAA LA VIONGOZI

### FILIPE JACINTO NYUSI

# Rais wa Msumbiji anayetishiwa hatima na waasi

## ▌Aziomba Ulaya, SADC kuokoa Cabo Delgado



Rais Nyusi akiwa kwenye majukwaa ya kisiasa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

KILICHOANZA kama mgogoro mdogo wa ndani nchini Msumbiji sasa kinainuka kuwa janga la kimataifa kikihitaji ushirikiano wa mataifa mbalimbali .

Ni magaidi wanaoishambulia Msumbiji kwenye jimbo la Cabo Delgado, lililo mpakani na Tanzania mkoani Ruvuma.

Rais wa nchi hiyo Filipe Jacinto Nyusi, akiwa kiongozi wa awamu ya nne ya taifa hilo, ndiye anayepambana na changamoto hiyo ambayo imekuwa pasua kichwa kwa eneo zima la Kusini mwa Afrika.

Nyusi aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kusini mwa Afrika (SADC) kuanzia Agosti 2020, ameomba msaada kukabili magaidi hao.

Tangu alipoingia madarakani Rais Nyusi, amekuwa mtetezi mkuu wa amani na kuimarisha usalama na amesaini mikataba mingi na makubaliano ya kuwa na amani baina yake na wapinzani wake wakuu chama cha RENAMO.

Nyusi aliwahi kuwa Waziri wa Ulinzi mwaka 2008 hadi 2014 wakati huo nchi hiyo ikiongozwa na Rais Armando Guebuza. Ilipofika 2014 alichaguliwa kuwa Rais kadhalika 2019 alipata tena ushindi na kuendelea kuliongoza taifa hilo.

Nyusi ameona kuwa hali ya Msumbiji si shwari na sasa ameomba msaada wa kimataifa kukabiliana na waasi wanaoendesha shughuli zao katika Jimbo la Cabo Delgado.

Mkakati wake wa kufurumusha makundi ya waasi ambayo yanaichachafya Cabo Delgado, jimbo lenye eneo kubwa zaidi nchini Msumbiji upande wa kaskazini, umeanza kuungwa mkono.

Nchi za Ulaya na Marekani zimeonyesha nia ya kusaidia kumaliza uasi katika eneo hilo lenye utajiri wa gesi.

Vyombo vya habari vya kimataifa vinasema kuwa tayari Ureno imepeleka platuni mbili na Ufaransa kikosi kimoja wote wakijiandaa kuisaida Msumbiji kukabili uasi huo.

Marekani ambayo ilikuwa inangojewa zaidi kutoa jibu kuhusu suala hilo kwani tayari inakamilisha kuondoa vikosi vyake nchini Afghanistan ila kutoa msaada wa mashambulizi ya anga kuzuia kutekwa nchi yote na Taliban, imesema itapeleka wataalamu wa kufundisha vikosi vya jeshi la Msumbiji.

> Mjadala uliosikika katika vyombo vya habari vya kimataifa ni kama mfungamano huo wa kuisaidia Msumbiji utafaulu, kwani katika nchi nyingi uasi kama huo umekuwa ukisambaa na kuwa ni tatizo la kudumu, lililoota mizizi.

Siyo jambo la kushangaza kuwa Ufaransa inaongoza katika suala hilo kwani kampuni yake ya mafuta ya TOTAL ina mradi mkubwa wa kuzalisha gesi asilia (liquefied naturall gas) ambao sasa umefikia hatua kubwa na ni wa uwekezaji mkubwa.

Mjadala uliosikika katika vyombo vya habari vya kimataifa ni kama mfungamano huo wa kuisaidia Msumbiji utafaulu, kwani katika nchi nyingi uasi kama huo umekuwa ukisambaa na kuwa ni tatizo la kudumu, lililoota mizizi.

Ila ni lazima kukiri kuwa siyo kila mahali magaidi wameweza kukamata eneo na kumiliki, kwani kwa sehemu kubwa inategemea mizizi waliyonayo katika eneo husika, na hapo siyo kila mchambuzi wa habari au mshauri wa mamho ya nje anaweza kusema kwa uhakika nini kinahusika Msumbiji.

Ni tatizo mojawapo lililokwamisha nchi za Jumuia ya Maendeleo Kusini ya Afrika (SADC) kupanga mkakati wa kuingilia kati, wakihofia vita kubwa na hata kuisambaza katika nchi wanachama.

Moja ya maeneo ambayo yanalinganishwa na tatizo la Cabo Delgado ni Somalia, hasa kwa vile kundi hilo linajitambulisha kitikadi na Al Shabaab, lililochipuka kutoka Al Qaeda na kimsingi ni moja ya matawi yake.

Tofauti ni kuwa kuna mparaganyiko wa kiitikadi na kisiasa nchini Somalia ambao unakuwa nguzo ya kundi hilo kujijenga ndani ya nchi, kwani halihitaji kutumia nguvu nyingi ili watu wawatii, kwa mfano juhudi zinazotumiwa na makundi ya kigaidi katika nchi za Afrika 'magharibi ya Somalia.'

Halafu kundi la Msumbiji halina uwanja mpana kujificha na kuendeleza operesheni, kama Al Shabaab.

Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro, alieleza miezi michache iliyopita kuwa kundi hilo ni lile lile lililoanza machafuko maeneo ya Mkoa wa Pwani na Lindi, likafurumishwa ndipo likahamisha maskani na kutua Msumbiji.

Ukiangalia maneeo hayo yanafanana, yana wakazi wanaoendana kwa lugha au utamaduni na dukuduku za hapa na pale dhidi ya serikali, kwa mfano 'kuna utajiri wa mafuta lakini wananchi ni maskini,' na wakati mmoja baadhi ya wanaoyapuuza makundi kama hayo wakasema walichukizwa na kukataliwa kukata mikoko maeneo ya bonde la mto Rufiji.

Kwa hasira hiyo walianzisha vita, walipue nchi.

Suala la gesi hapa nchini lilileta chokochoko kwa mfano mwaka 2013 kukatokea maandamano mjini Mtwara, kundi la watu limebeba mabango kuhusu gesi, baadhi wakatoa dhihaka, 'shemeji gesi haitoki,' ikabidi Rais Jakaya Kikwete atoe tadhadhari, 'nitawapelekea vita.'

Kungekuwa na mparaganyiko zaidi nchini wangeweza kujikita katika maeneo ya mbuga za mikoa hii ya Pwani, na mwelekeo ungekuwa kuzingira mitambo ya gesi kama wanavyofanya Msumbiji.

Ila tatizo linabaki pale pale, lile aliloainisha Waziri wa Mambo ya Nje, Liberata Mulamula hivi karibuni, kuwa 'hujui unapambana na nani, au yuko wapi...

Kinacholeta picha ya matumaini kiasi fulani ni kuwa licha ya kuwa dola Msumbiji limejukita zaidi maeneo ya kusini na mbuga za kaskazini ya nchi zina uhaba wa uwepo halisi wa serikali, serikali haina mparaganyiko wa kisiasa kuzuia kusonga mbele, endapo kunakuwapo hali bora zaidi ya uwezeshaji, kujenga ari miongoni mwa wapiganaji na makamanda kuwa mapambano hayo yanaweza kufikia tamati hitajiwa katika muda mfupi kiasi. Sababu ya uwepo wa tumaini ni kuwa hasa kinachotakiwa ni kudhibiti nyendo za magaidi na ngome zao eneo la pwani (kwa mfano mji wa Pemba ambao una bandari), halafu kufuatilia njia za panya na maskani porini, kwa upana wa jimbo hilo lote.

Haitakuwa kazi ndogo kwani ni kama kupekua eneo lote la mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ili kufurumisha magaidi, lakini endapo hawawezi kuhamia kwa muda maeneo mengine na kurudi tena baadaye, wanaweza kukomeshwa.



# H'shauri 8 zafanya ukaguzi usalama wa chakula

Na Renataha Msungu, DODOMA

HALMASHAURI nane mkoani hapa, zimefanya ukaguzi wa usalama na ubora wa chakula ili ziweze kujua ubora ikiwamo kubaini uwapo wa vyakula vilivyokwisha muda wake.

Ofisa Lishe wa Mkoa, Carren Heriet, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu suala la lishe katika mkoa wa Dodoma.

Carren, alizitaja halmashauri hizo ni pamoja na Bahi, Chamwino, Chemba, Dodoma Jiji, Kondoa, Kondoa Mji, Kongwa na Mpwapwa.

Alisema halmashauri hizo zote zilifanikiwa kufanya kaguzi za vyakula na kupata asilimia 100 na mwitikio umeonekana mzuri na umefanyika ipasavyo.

Alisema halmashauri hizo zilifanya usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na masuala mbalimbali yanayohusu lishe, ikiwamo utekelezaji wa shughuli mbalimbali za usimamizi shirikishi katika ngazi za halmashauri.

Alisema mkoa utaendelea kufuatilia halmashauri zilizotoa fedha pungufu ili kuhakikisha inatoa fedha kulingana na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe toka katika vyanzo vya mapato ya ndani.

Katika hatua nyingine alizungumzia utoaji wa vidonge vya madini ya chuma na kwamba katika kipindi

cha ujauzito ni kipindi ambacho vinahitajika kwa wanawake wenye hali hiyo ili kuhakikisha wanakuwa salama.

Alisema madini ya chuma ni muhimu katika kipindi cha ujauzito kwa sababu huzuia tatizo la upungufu wa damu kwa wajawazito.

Alifafanua kuwa halmashauri kupitia vituo vya kutolea huduma za afya hutoa elimu ya matumizi ya vyakula vya kuongeza damu kwa wajawazito pamoja na kutoa nyongeza ya vidonge vya madini ya chuma na Folic acid.

Aidha, alisema kinamama 64,471 kati ya 73,702 waliohudhuria kliniki walipewa vidonge vya madini ya chuma na folic acid sawa na asilimia 87.

Alisema vituo vya kutoa huduma vitaendelea kufuatilia la utoaji vidonge vya madini ya chuma ili kuhakikisha wajawazito wanakuwa katika hali ya usalama katika kipindi hiko hadi kujifungua.

# Jukwaa la wachambuzi kujadili upungufu kisera

Na Paul Mabeja, DODOMA

JUKWAA la wachambuzi wa sera katika sekta ya kilimo nchini (PAG), limeandaa kongamano la siku tatu kujadili upungufu wa kisera unaokwamisha ukuaji wa sekta ya kilimo nchini.

Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Audax Lukonge, alisema kuwa kongamano hilo la saba litafanyika kwa siku tatu kujadili mambo mbalimbali ya kisera katika sekta hiyo ya kilimo.

Alisema litahusisha watunga sera, watafiti, wadau wa maendeleo wanataaluma mbalimbali na wazalishaji wa bidhaa nchini.

Alisema katika kongamano hilo washiriki watapata fursa ya kujadili kwa pamoja na kupata majibu ya kero mbalimbali ambazo zipo kisera katika sekta ya kilimo.

"Katika kongamano hili washiriki watapata fursa ya kujadiliana mambo mbalimbali ya kisera katika sekta ya kilimo na kubadilishana uzoefu ili kusaidia kuondoa changamoto zilizopo katika kilimo nchini," alisema Lukonge.

Alisema pamoja na mambo mengine pia washiriki watapata fursa ya kufanya mapendekezo ya maboresho ya kisera ili kufanya Tanzania kuingia katika ushindani wa soko la kikanda na la kimataifa katika sekta ya kilimo na mifugo.

"Pia katika kongamano hilo tutakwenda kuangalia kwa namna gani bidhaa zetu zinazozalishwa nchini zina uwezo wa kushindana katika soko la kikanda na kimataifa ili kutafuta majibu," alisema Lukonge. Vile vile, alisema wajumbe watajadili suala la uingizaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi ambazo zimekuwa zikitumia kiasi kikubwa cha fedha.

"Katika mafuta tu ya kula tunatumia takribani bilioni 500, kwa mwaka kiasi ambacho ni kikubwa sana sasa katika kongamano hilo kupitia wadau mbalimbali tutaona ni njia gani tunatumia ili kuondokana na changamoto hii," alisisitiza.

Pia alisema hivi sasa kumekuwapo na wimbi kubwa la uingizaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi hali ambayo inatakiwa kupatiwa majibu haraka.

Jacqueline Mkindi, mjumbe wa jukwaa hilo, alisema ili kuwa na kilimo chenye tija mambo makuu matano yanatakiwa kupatiwa kipaumbele.

Alisema moja kati ya mambo hayo ni upatikanaji wa ardhi ya kutosha, mitaji ya kilimo, uboreshaji wa miundombinu ikiwamo viwanja vya ndege, bandari, barabara pamoja na udhibiti wa upotevu mavuno shambani.

"Hili la upotevu wa mavuno shambani ni changamoto kwani hivi sasa mkulima anapoteza kiasi kingi cha mavuno kuliko kile kinachofika sokoni takribani asilimia 40 ya mavuno inapotea ikiwa shambani," alisema Mkindi.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kushoto), akipewa chanjo ya ugonjwa wa corona na muuguzi Fulgensia Mvulla wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katibu Tawala ataka elimu, afya, kilimo vipande

Na Renatha Msungu, DODOMA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, amewataka watumishi wa mkoa huo kuvaa sura za kazi ili kwenda kuinua sekta ya elimu, afya na kilimo.

Dk. Mganga aliyasema hayo juzi wakati wa kikao kazi cha viongozi watumishi wa mkoa wa Dodoma chenye lengo la kujadili mustakabali wa maendeleo ya mkoa.

Alifafanua kuwa katika suala la elimu Dodoma kuwa nyuma ni aibu kutokana na kwamba ni makao makuu kila kitu kinapatikana hususani bajeti ya fedha ambayo inatengwa na serikali katika kuendeleza sekta hizo.

Alisema watumishi wanapaswa kuondoka na lugha moja ya kuhakikisha wanakwenda kuinua sekta ya elimu katika maeneo wanayotoka ili Dodoma iwe juu katika sekta ya elimu na sekta nyingine ambazo ni muhimu kwa jamii.

"Nawaomba watu muende kuvaa sura za kazi, acheni masihara kafanyeni kazi Dodoma ijulikane kwa kila kitu," alisema Dk. Mganga.

Akizungumzia suala la afya, Dk. Fatuma alisema wanahitaji kuona tatizo la udumavu, upungufu wa uzito na utapiamlo mkali vinatokea katika mkoa huo.

Alisema kama fedha ipo na inatolewa katika bajeti kwanini udumavu uwapo ilhali wataalamu wapo.

Katika suala la kilimo aliwataka wataalamu wa kilimo kuhakikisha wanasimamia kilimo cha zabibu ambacho kinastawi vizuri mkoani humo.

Alisema hivi karibuni Waziri Mkuu alipokutana nao, aliwataka kuhakikisha zao la zabibu linakuwa la kimkakati kwa sababu linafaida nyingi linapovunwa kutoka katika mashamba ya wakulima.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema moja ya vipaumbele vyake katika utendaji ni suala la elimu na kwamba watumishi wanapaswa kwenda kuzingatia katika suala la kuinua kiwango cha elimu.

Alisema elimu ndio mtaji wa wanafunzi, ndio maana kila siku amekuwa akipiga kelele wanafunzi kuonekana wanazagaa zagaa mtaani badala ya kuwapo shuleni.

Mtaka alisema anataka kuona Dodoma inakuwa juu katika elimu na vitu vingine na kwamba ni vyema watumishi washikamane kuhakikisha mkoa unasonga mbele kielimu na kushika nafasi za juu katika mitihani ya kitaifa.



# Majaliwa ataka vyuo vya ufundi kufundisha Kiswahili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza mafunzo ya uanagenzi yanayotolewa kwa vijana katika vyuo mbalimbali vya ufundi nchini kutolewa kwa lugha ya Kiswahili ili wanufaika wote waelewe kwa urahisi wanachofundishwa.

Alitoa agizo hilo juzi jijini hapa alipokuwa anazindua rasmi mafunzo hayo ya uanagenzi awamu ya tatu na kutaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusimamia utaratibu huo ili malengo ya serikali ya kuongeza ujuzi kwa vijana yatimie.

Mafunzo hayo yanafadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kutengeneza fursa za ajira 8,000,000 ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana pamoja na kukabiliana na tatizo la uhaba wa wataalamu.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa hata kwa vijana ambao waliishia darasa la saba na hawajui kabisa Kiingereza na kuwafundisha kwa lugha ambayo hawaijui ni kutowatendea haki na kuna uwezekano malengo ya serikali yasitimie.

Alisema mafunzo hayo pia yanalenga kuliwezesha taifa kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025 ya kufikia uchumi wa kati wa juu tofauti na ilivyo sasa taifa limefikia uchumi wa kati wa chini.

"Naagiza Wizara ya Elimu kuhakikisha mitaala yote ya mafunzo haya iandaliwe kwa lugha ya Kiswahili ili vijana wetu wote wanaojifunza ufundi huu waelewe, hapa kuna wengine waliishia darasa la saba na wengine walishindwa kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu mbalimbali kwa hiyo Kiswahili ni muhimu kitumike," alisema Majaliwa.

Aliwataka vijana wanaonufaika na mafunzo hayo kusoma kwa nguvu ili watimize ndoto zao za kupata ujuzi ili waje waitumie kujiinua kiuchumi kwa kujiajiri wao wenyewe ama kuajiriwa.

Aliziagiza halmashauri kushiriki kwenye utekelezaji wa mafunzo hayo kwa kuwatambua vijana wanaopata mafunzo hayo ili ikiwezekana wapewe kipaumbele kwenye mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kuwakopesha.

Alisema kabla ya kuzindua mafunzo hayo alifanya ziara kwenye vyuo vinavyotoa mafunzo hayo ambavyo ni Chuo cha Ufunzi Stadi (VETA) Busokelo na Chuo cha Kyela Polytechnic (KPC) na kushuhudia vijana wakiwa wanatengeneza vitu mbalimbali licha ya kujifunza mwezi mmoja pekee.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa muda wa miezi sita na tangu yalipoanza yamefanyika awamu mbili ambazo zimewanufaisha vijana 28,941.

Alisema mafunzo hayo yanamhusisha mhusika kutumia asilimia 40 ya muda anaokuwa chuoni kujifunza kwa nadharia darasani na asilimia 60 ya muda anautumia kwa masomo ya vitendo sehemu ya kazi.

Waziri Mhagama alisema baada ya vijana hao kuhitimu mwezi Desemba mwaka huu, idadi ya wanufaika wa programu hiyo ya kukuza ujuzi nchini itafikia 80,320 na kuwa na nguvu kazi ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi pamoja na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Alisema katika mafunzo hayo vijana hao hawalipii gharama yoyote kwa kwa kuwa asilimia 100 ya gharama zote inagharimiwa na serikali na kijana akiombwa chochote na mtu yeyote ili awe miongoni mwa wanufaika itatafsiriwa kuwa ni rushwa.

"Mafunzo haya yanatolewa katika vyuo 72 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na yanatolewa kwa kuzingatia miongozo ya Shirika la Kazi Duniani na kabla ya kuanza kutolewa yalishafanyiwa utafiti na kupimwa kwenye maabara ya kimataifa," alisema Mhagama.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akiteta jambo na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uanagenzi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), jijini humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mbunge apendekeza chakula cha mchana kwa wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, ameshauri Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuweka mikakati ya kuhakikisha lazima chakula cha mchana kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kinapatikana ili kuongeza ufaulu.

Mwakagenda alitoa kauli hiyo juzi, wakati akizungumza na Nipashe ambapo alisema ajenda ya chakula shuleni ni vyema ikatekelezwa kwa asilimia 100 ili kupata matokeo mazuri kwa watoto na kuipa sifa nzuri wilaya hiyo.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa na mwamko mdogo katika uchangiaji wa chakula shuleni na kwamba ni jukumu kwa watendaji wa wilaya kuhamasisha chakula kipatikane ili watoto waendelee kusoma kwa utulivu na kujiongezea maarifa. "Naishauri Wilaya ya Rungwe tuibebe ajenda hii ya watoto kula chakula shuleni, utekelezaji wake bado unasuasua hauwezi kuinua kiwango cha ufaulu namna hii endapo sisi wenyewe hatutaweka mikakati ya kuwahamasisha wazazi kuchangia chakula au kutenga sheria ndogo zinazombana mzazi achangie," alisema Mwakagenda.

Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Anthony Mwantona, alisema kupatikana kwa chakula shuleni ni njia mojawapo itakayoweza kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Alisema ataendelea kufanya vikao na watendaji pamoja viongozi wa vijiji na vitongoji ili kupata mbinu ya kuhamasisha wazazi au walezi kuona umuhimu wa kuchangia chakula shuleni.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema kiwango cha ufaulu katika wilaya hiyo bado hakiridhishi na kuwaagiza viongozi wa halmashauri kujituma na kubuni njia mbalimbali za kuongeza ufaulu.

Alisema hali ya hewa ya wilaya hiyo inavutia kwa mwanafunzi kupata utulivu wa kujisomea na kufanya vizuri kwenye mitihani yake, lakini miongoni mwa vikwazo ni kukosekana na mikakati ya namna ya kuongeza ufaulu.

"Nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti nilikutana na tatizo kama hilo ufaulu mdogo tena kule ilikuwa zaidi tukafanya vikao na kuweka mikakati kila mmoja alipewa majukumu yake kuhakikisha wastani wa ufaulu kwa kila mwanafunzi unaongezeka huku chakula kikiwapo shuleni tulifanikiwa," alisema Dk. Anney.

Diwani wa Viti Maalum Masoko, Anna Kilasa, alisema uelewa kwa wanafunzi kwa sasa umekuwa mdogo ikilinganishwa na kipindi ambacho walikuwa wanasoma.

Alidai kwa sasa mwanafunzi anashindwa kujibu maswali ya darasa la nyuma huku wastani wa ufaulu katika masomo yake ukiwa mdogo licha ya baadhi yao pia kuongoza kwa mazingira hayo.

Aliishauri kamati za shule na waratibu wa elimu kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kupima uelewa wa wanafunzi na kubaini upungufu ili wayashughulikie.

## Serikali yahakikisha kuboresha vituo vya afya

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI imewahakikishia wananchi, kuendelea kujenga na kuboresha vituo vya afya na miundombinu ya elimu ili wananchi wapate huduma hizo kwa wakati na urahisi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Kyela kuwa serikali imeendelea kujenga vituo vya afya kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo na kuwasaidia wananchi kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

Alisema serikali pia inaendelea na ukarabati pamoja na ujenzi wa miundombinu ya elimu kuanzia shule za msingi na sekondari na lengo ni kuhakikisha watoto wanasoma kwenye mazingira mazuri ili waweze kutimiza malengo yao.

"Nawahakikishia wananchi wote kwamba serikali kupitia TAMISEMI inaendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa shule zikiwamo maabara za kisasa kwa ajili wanafunzi wetu kufanya mazoezi ya vitendo vilevile tunaendelea na ukamilishaji wa miundombinu mingine ili mazingira ya upatikanaji wa elimu yawe mazuri kuchagiza ufaulu," alisema Silinde.

Aliwaomba wananchi kwa kushirikiana na serikali kuendelea kutoa nguvu kazi zao ili kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na kuondoa adha ya watoto kukosa sehemu ya kujisomea kutokana na udahili au ufaulu wa wanafunzi.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Kinanasi, alisema bado kuna uhaba mkubwa wa vituo vya afya na zahanati na kwamba wananchi hulazimika kutumia umbali mrefu kufuata huduma za afya na wakati mwingine kutumia gharama kubwa kufika hospitali ya wilayani.

Aliiomba serikali kuendelea kuisaidia wilaya hiyo ili kujengewa vituo vya afya wananchi wapate huduma karibu na maeneo yao na kuendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Suma Fyandomo, aliiomba serikali kuendelea kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto ili kuepukana na vifo wakati wa kujifungua.



# SMZ yaahidi ushirikiano kwa waratibu wa sensa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewahakikishia viongozi wenye dhamana ya usimamizi wa sensa nchini kuwa Serikali ya Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha inafanyika vizuri muda utakapowadia.

Hemed aliyasema hayo jana ofisini kwake Vuga alipozungumza na Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Mohamed Hamza, alipofika ofisini kwake akiambatana na vingozi kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa ajili ya kujitambulisha.

Makamu wa Pili wa Rais aliwataka viongozi hao kuendelea kutoa elimu na kuihamasisha jamii kupitia ngazi zote kwa kuwatumia viongozi mbalimbali kwa lengo la kuwaweka wananchi tayari kuhesabiwa muda utakapofika.

Alisema sensa hiyo ambayo hufanyika kila baada ya miaka 10 ina umuhimu mkubwa katika kufahamu idadi ya watu wake na kuisaidia serikali kupanga mikakati yake ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi wake.

Hemed aliutaka uongozi huo kuendelea kuainisha vikwazo mbalimbali vinavyowakabili na kuziwasilisha serikalini ili kupatiwa ufumbuzi kwa wakati stahiki.

"Ninapenda kuwahakikishia ushirikiano wangu, nipo tayari kushirikiana nanyi muda wowote mtakaponihitaji ili kufanikisha azma ya zoezi la kujua idadi ya watu wetu," alisema.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Hamza, alisema kutokana na sensa kuwa tegemeo kwa taifa, atahakikisha nafasi aliyokabidhiwa anaitendea haki.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mayasa Mahfoudh Mwinyi, alisema ofisi yake imejipanga vyema kuendesha sensa na tayari imeandaa dodoso za ngazi tofauti ili kutoa fursa kwa ngazi hizo kushiriki katika sensa ya watu na makazi.

Aliema majaribio ya sensa ya watu na makazi yatajumuisha maeneo 10 katika mikoa yote ya Zanzibar.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (katikati), akizungumza na viongozi kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakiongozwa na Kamisaa Balozi Mohamed Hamza aliyeteuliwa hivi karibuni alipofika ofisini kwake Vuga jana, kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## BAWACHA walaani viongozi kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BARAZA la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Zanzibar, limesema linasikitishwa na kulaani vikali vitendo vya kukamatwa kwa viongozi, akiwamo mwenyekiti wa chama hicho.

Limesema linaamini kukamatwa huko kwa viongozi wake ni sehemu ya mikakati ya kisiasa inayolenga kuzuia juhudi za chama hicho kupigania haki za watu na utawala wa sheria.

Kaimu Mwenyekiti wa baraza hilo, Sharifa Suleiman, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho huko Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema suala la Katiba Mpya na Tume huru ya uchaguzi ndio hitaji lao kwa demokrasia na pia kwa mustakabali mwema wa taifa na maisha ya watu.

Kiongozi huyo alisema: "Mtakumbuka pamoja na kutiwa nguvuni mwenyekiti wetu, viongozi kadhaa wa chama walikamatwa na kuwekwa rumande kinyume cha sheria."

Alidai mtiririko wa matukio hayo unaonekana wazi kulenga kuwadhibiti kupigania matakwa ya umma juu ya uhitaji wa Katiba Mpya na utawala bora wa kisiasa na kiuchumi nchini.

Alimshauri Rais wa Tanzania kutafakari upya mwenendo wa siasa nchini na hatima njema ya Tanzania.

Hata hivyo, uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi nchini ulitoa tamko hivi karibuni kuhusu madai yao ya CHADEMA, ukisisitiza kuwa kukamatwa na kushtakiwa kwa baadhi ya viongozi wao kunafanyika kwa mujibu wa sheria na sio vinginevyo.

# Bodaboda wapewa angalizo la corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Waendesha Bodaboda Zanzibar, Amiri Mussa Muhidini, amewataka madereva wa usafiri huo kuchukua tahadhari za kujikinga na corona kutokana na kusafirisha watu wa aina tofauti.

Akizungumza jana na Nipashe kisiwani hapa, mwenyekiti huyo alisema miongoni mwa tahadhari ambazo wanapaswa kuzichukua ni kuvaa barakoa na kutembea na vitakasa mikono.

Alisema ni vyema kuhakikisha wanavaa barakoa na kutembea na vitakasa mikono kwa ajili ya kuosha mikono yao pamoja na wateja wao ili kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Ninawaasa madereva wezangu tuwe makini maana ugonjwa wa corona upo na sisi kazi yetu hii tunasafirisha watu wa aina tofauti," alionya. Mwenyekiti huyo pia aliyataka mashirika mbalimbali pamoja na watu wenye uwezo ambao wanatoa msaada wa vifaa vya kujikinga na corona, kulikumbuka kundi la madereva bodaboda kwa misaada hiyo.

"Tunaomba na sisi tupatiwe msaada wa vifaa vya kujikinga na corona ikiwamo barakoa na vitakasa mikono," alisema.

Hata hivyo, aliwataka madereva wa usafiri huo ambao sasa umesharasimishwa na serikali kufuata marejeo ya sheria, kuzingatia sheria ili kuepuka ajali zisizo za lazima.

Wananchi wanaotumia usafiri huo, walisema kuwa bado tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona ni ndogo tofauti na mwanzoni ugonjwa huo ulipoingia nchini.

Amina Makame, alisema tahadhari hiyo imekuwa ndogo kutokana na wananchi wengi kutokuwa na hofu dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema bado elimu zaidi inahitajika kuhusu tahadhari ya corona katika kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mwananchi huyo alisema tayari Tanzania Bara wameshaweka masharti ya ulazima wa uvaaji wa barakoa katika usafiri wa umma ikiwamo daladala lakini kwa Zanzibar bado na watu wanatembea na kukutana katika mikusanyiko mbalimbali bila ya kuvaa barakoa.

Hata hivyo, tayari Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, ameshawasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Waziri huyo alibainisha hivi karibuni kuwa tayari watu wanane wameshagundulika kuwa na corona katika wimbi la tatu la ugonjwa huo na wanaendelea kupatiwa matibabu.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

IPO PUGU KAJIUNGENI, ZIPO MBILI. MOJA HAIJAMALIZIKA, FREMU SITA ZA BIASHARA INA OFFER. BEI NI MIL. 65.

KWA MAWASILIANO:

0787 – 608011 / 0762 944949.

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAUSTA FRANCIS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1373-0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MBELEI SEKONDARI mwaka 2014. Y**eyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **WMB/RB/459/2021.**

11639002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YAN KINONDONI**
**Misc.Civil Application NAMBA 126 YA MWAKA 2021**
**AMINA MAUNDU……..MDAI**
**DHIDI YA**
**SIGSBERT PATILA MKUDE…..MDAIWA**
**KWA.**
**SIGSBERT PATILA MKUDE**
**DSM**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya madai ambayo yanaweza kupatikana katika mahakama hii,kwahiyo unahitajika kuhudhuria mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa siku ya jumatano tarehe 18 mwezi 8 mwaka 2021 saa 2:00 asubuhi

Kwa mujibu wa maombi hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO.**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitika kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa .

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 08 mwaka 2021.

11639102

**CHAMA CHA WAHASIBU TANZANIA (TAA)**
**TANGAZO LA KUPOTEA**
**KWA CHETI CHA USAJILI WA CHAMA**

Chama cha Wahasibu Tanzania **(TAA)** kinautangazia Umma kuwa kimepotelewa na Cheti cha Usajili wa Chama chenye namba **So.No. 6321.** Yeyote atakae kiona anaombwa kukiwasilisha kwenye ofisi za **TAA** zilizopo mtaa wa Bibi Titi Mohamed-Mhasibu House, Dar es Salaam.

**Au kwa kupiga simu namba**
**0769-167278/0787-464523**
**IMETOLEWA NA**
**Baraka Aambangile**
**Mtendaji Mkuu**
**CHAMA CHA WAHASIBU TANZANIA**

11639202

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 79 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**LATE: PETER AYUBI KITUNDU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**DR. JESSE KITUNDU**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 26 Mwezi wa 08, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 22 Mwezi wa 7, 2016.**

NAIBU MSAJILI

11639302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLEMENT ELIAKIM KIDALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CRESTA** yenye namba za usajili **T 293 ANV** chasisi namba **GX1006007807** engine namba **IG6426110,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**DSM/PHQ/RB/ 370007/2021**

11639402

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**(SURA YA 113)**
**KUHAMISHA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA :HAMADI KULELE**
**KWENDA KWA :MICHAEL MASOTA**
**ARDHI:KIWANJA NA(4) KWA SASA NI NAMBA 434 KITALU J**
**ENEO LA MBAGALA**
**MANISPAA YA TEMEKE JIJINI**
**DAR ES SALAAM**

Taarifa inatolewa kwamba **AFISA ARDHI MTEULE** anakusudia kuhamisha **BARUA YA TOLEO TAJWA YA KUMILIKI ARDHI** kwenda kwa **MICHAEL MASOTA** aliyewasilisha barua ya toleo pamoja na mkataba wa manunuzi kwamba ameuziwa kiwanja hicho,ikiwa kwa jina la **HAMADI KULELE.** Ninakusudia kutoa **HATI MILIKI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti.

P.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

116378002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**OMARI HAMISI BINDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **MITSUBISHI PICK-UP** yenye namba za usajili **T 815 BHE.Chasis No. FE638E502089,** Engine **No 4D35585544** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/381865/2021.**

11639102

## KUPOTEA KWA CHETI



**Kulwa Makenzi** anatangaza kupotelewa kwa cheti chake chuo ngazi ya diploma chuo cha Udom university of Dodoma ,kilichotolewa mwaka 2019 namba ya usajili ya cheti ni **D.MEDLAB 00004686.** yeyote atakayekiona cheti hicho atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu.

**Taarifa ya polisi SIM/BAR/RB 353591/2021.**

116391202

**GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED**
**Head Office:** P.O.BOX 40855 Dar es Salaam - Pugu station Bangulo
Branch: Mkombozi Bank Agrey Street - Kariakoo/ Mwanza Rufiji Street
Branch: Kilombero Ruaha Morogoro
Email:gadauauctionmart@gmail.com/gadauauctionmart@yahoo.com
hashimugadau@yahoo.com

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI LOTE**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA CRDB** tutauza kwa mnada wa hadhara **DHAMANA MBALIMBALI ZA WADAIWA WA TAASISI HIYO.** Minada itafanyika kuanzia tarehe 18/8/2021 HADI Ukomo mahali zilipo dhamana.

**UFUATAO NI MCHANGANUO WA MAJINA YA WADAIWA, DHAMANA NA MAHALI ZILIPO:**

| Na. | JINA LA MTEJA | TAWI | DHAMANA INAYOUZA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PASCAL ANSELM LYARUU | KIBAHA | CT.NO. 148557, LO.NO. 519656, PLOT NO. 1, BLOCK T, VISIGA, KIBAHA MJINI | VISIGA, KIBAHA MJINI | 18/8/2021 **5:00 asubuhi** |
| 2 | MARIAM AMULIKE KIBONA | MBEYA | CT. NO. 21093-MBYLR, LO.NO. 378177, PLOT NO. 292, BLOCK A, UYOLE, MBEYA | UYOLE, MBEYA | 18/8/2021 **5:00 asubuhi** |
| 3 | EVA HILARY KIWILI | MZUMBE | NYUMBA KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA KILICHOPO BIGWA SOKONI, KILAKALA – MANISPAA YA MOROGORO | BIGWA SOKONI, KILAKALA - MOROGORO | 18/8/2021 **4:00 asubuhi** |
| 4 | FRANK ANAKLETI JOSEPH | MZUMBE | KNYUMBA KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA KILICHOPO MAENEO YA KOLOLO-MELELA, WILAYA YA MVOMERO | KOLOLO-MELELA, MVOMERO | 21/8/2021 **5:00 asubuhi** |
| 5 | DIDAS DOMINIC CHAMI | MZUMBE | KNYUMBA KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA KILICHOPO MAENEO YA KILIMANJARO, KIHONDA MOROGORO | KILIMANJARO, KIHONDA MOROGORO | 18/8/2021 **6:00 mchana** |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana,
2. Mnunuzi atakayefikia bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano 25% ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano 75% atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya m nada.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.

**WOTE MNAKARIBISHWA**
**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**GADAU AUCTION MART AND COMPANY L.T.D**
**S.L.P 40855, DAR ES SAALAM, SIMU; 0714 635599/ 0785 636864**

216391502

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MOSHI**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI**
**SHAURI NAMBARI 9 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**FRANK SAWAYA MAWALLA……………………MAREHEMU**
**DHIDI**
**PRAYGOD FRANK MAWALLA…………………WAOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 Mwezi wa SEPTEMBA, Mwaka 2021.

Imewasilishwa Moshi leo tarehe 19 Mwezi wa JULAI, Mwaka 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU MOSHI

116391302




**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB:+255 - 0782253676**

## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waziri Lukuvi kuwanyang'anya ardhi wasioendeleza

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema mwekezaji yeyote aliyechukua eneo na hajaliendeleza kwa miaka 10 utaratibu wa kunyang'anywa utafanyika ili wapewe watu wengine.

Pia amesema mwekezaji yeyote atakayechukua fedha benki kwa ajili ya kuendeleza eneo alilochukua, anatakiwa kufanya hivyo na akienda kinyume benki inatakiwa kumbana atafute dhamana nyingine na si ya ardhi.

Alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akikagua mradi wa ujenzi wa kiwanda cha sukari na shamba la miwa lililopo Bagamoyo, mkoani Pwani.

Alisema wapo watu wamepewa ardhi, lakini hawajaiendeleza pamoja na kulipa kodi zinazotakiwa serikalini, hawataendelea kuvumiliwa kuacha maeneo hayo kwa muda mrefu.

"Unafanyika ukaguzi ambao hawajaiendeleza maeneo yao kwa miaka 10 yatarudi serikalini wapewe wawekezaji wanaoweza kufanya hivyo kwa haraka, baadhi yao wanachukua ardhi kwa ajili ya kukopea tu," alisema Lukuvi.

Pia, amewaagiza Makamishna wa Ardhi ngazi ya mikoa waanze utaratibu wa kunyang'anya mashamba ambayo hayajaendelezwa ili wanaoomba ardhi ya kuwekeza wapate.

Alimpongeza Bakhresa kwa kuitikia wito wa serikali kukubali kujenga kiwanda cha sukari kupunguza kero ya uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Alisema wamekubaliana na Mkuu wa mkoa kukutana na mawaziri ambao wanahusika kufikisha huduma kwenye mradi huo watakutana nao kujadiliana kuhakikisha malengo ya Bakhresa katika mradi huo yanafikiwa.

Serikali ya awamu ya tano ilimpatia Bakhresa hekta 10,000 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho na katika awamu ya kwanza uzalishaji unatarajiwa kuanza mwaka 2022.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema uwekezaji uliofanywa na Bakhresa katika mkoa huo ni kati ya miradi mikubwa ambayo ataendelea kuwa karibu nayo kuhakikisha hakuna kikwazo kinachoukwamisha.

"Tutaangalia vikwazo vilivyopo tusaidie kuviondoa, serikali ya mkoa itaendelea kutoa ushirikiano kwa asilimia 100 mradi ukamilike kwa wakati," alisema.

Kunenge aliwataka wawekezaji kufika kuwekeza kwenye mkoa huo ambao mazingira yake ni salama na yapo maeneo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji.

Mratibu wa mradi huo, Hussein Sufian, alisema ujenzi wa kiwanda kwa sasa umefikia asilimia 95 utakamilika mwezi Desemba mwaka huu, ufungaji wa mitambo tayari umeanza.

# Masharti ya kunyonyesha ukipata corona

**Na Mary Geofrey**

WAKATI taifa likiendelea na utoaji wa chanjo, imeelezwa kuwa mama mwenye maambukizi ya virusi vya corona hawezi kumwambukiza mtoto pindi anapomnyonyesha.

Uchunguzi wa Nipashe kupitia vyanzo vya kimataifa, likiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO) na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), umehakikishiwa hakuna uhusiano kati ya unyonyeshaji maziwa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na maambukizi ya corona.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Mkurugenzi wa Mafunzo na Elimu Lishe kutoka TFNC, Dk. Ester Nkuba, alisema: "Maziwa ya mama mwenye ugonjwa wa virusi vya corona ni salama kwa mtoto wake, anashauriwa kuendelea kunyonyesha kwa kuzingatia tahadhari za kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa majisafi tiririka na sabuni na kukaa karantini wakati akiendelea kunyonyesha."

Mtaalamu huyo alikumbusha mama anayenyonyesha anapaswa kuzingatia mlo kamili na kwa wakati, unaojumuisha makundi matano muhimu ya lishe.

Dk. Ester alitaja sehemu ya mlo huo unajumuisha maji, matunda, mboga za majani, nafaka, mizizi, mafuta na nyama.

WHO katika taarifa yake kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu, Dk.Tedros Adhanom, inaeleza kuwa kinamama wanatakiwa kuhakikisha unyonyeshaji unaendelea kwa sababu ni salama kwa mtoto.

Dk. Adhanom anasema ni uzushi kuwa kunyonyesha kunaweza kusambaza virusi vya corona kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na badala yake wananchi waendelee kuhimiza unyonyeshaji watoto.

"Katika nchi nyingi, janga hili limesababisha usumbufu mkubwa katika huduma za msaada wa kunyonyesha, huku likiongeza hatari ya ukosefu wa chakula na utapiamlo.

"Nchi kadhaa zimeripoti kuwa wazalishaji wa vyakula vya watoto wameongeza hatari hizi kwa kutumia hofu isiyo na msingi kwamba kunyonyesha kunaweza kusambaza ugonjwa wa corona na kutangaza bidhaa zao kama njia mbadala salama ya kunyonyesha," alisema mkuu huyo wa WHO.

Aliwakumbusha waajiri wa kampuni kutenga maeneo rasmi ya kunyonyesha na kuwaruhusu kinamama kuwa na muda wakunyonyesha watoto wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Henrietta Fore, alisema unyonyeshaji ni msingi wa kujitolea.

"Kuanza kunyonyesha ndani ya saa ya kwanza ya kuzaliwa, ikifuatiwa na unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa miezi sita na kuendelea kunyonyesha hadi miaka miwili au zaidi ni ulinzi dhidi ya aina zote za utapiamlo wa watoto, pamoja na kuondoa kunenepa kupita kiasi," alisema Fore.

Kauli mbiu ya mwaka huu ya Wiki ya Unyonyeshaji ni 'Kinga Unyonyeshaji: Jukumu la Pamoja'.

Katika hatua nyingine UNICEF imetoa mwongozo wa unyonyeshaji katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Mwongozo huo umeeleza mambo kadhaa ikiwamo mama anayenyonyesha anaruhusiwa kupata chanjo ya corona na iwapo anahisi kuumwa anaruhusiwa kuendelea kunyonyesha mtoto kwa kutumia kikombe kisafi, anatakiwa kuzingatia miongozo yote ya usafi ikiwamo kunawa mikono.

Mwongozo huo umetanabaisha hakuna taarifa yoyote iliyoonyesha mtoto ameambukizwa ugonjwa wa virusi vya corona kutoka kwa mama anayenyonyesha, hivyo hata mama akibainika amepata maambukizi anatakiwa kuendelea kunyonyesha mtoto.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Biashara ya DCB, Zacharia Kapama (wa tatu kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa huduma mbalimbali mpya za kibenki kwa njia ya kidigitali za DCB pamoja na uboreshaji wa huduma nyingine za benki hiyo. Wengine (kutoka kushoto) ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Fortunata Benedict, Mkuu wa Kitengo cha Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, Francisca Francis na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MO Foundation yatoa mamilioni Muhimbili

**Na Romana Mallya**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohamed Dewji 'MO' ametoa msaada wa Sh. milioni 100 kusaidia watoto wenye saratani wanaohudumiwa na Tumaini la Maisha (TLM) asasi isiyo ya kiraia inayofanya kazi na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Msaada huo ulitolewa jana hospitalini hapo jijini Dar es Salaam na taasisi ya MO (MO Foundation) na kupokelewa na Mwenyekiti wa TLM na hospitali ya Muhimbili.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mwenyekiti na Mwanzilishi wa TLM, Gerald Mongella, alisema mwaka huu wanatimiza miaka 10 tangu kuasisiwa kwa taasisi hiyo.

Alisema TLM ndiyo taasisi pekee Tanzania inayoshughulika na watoto wenye saratani na ilianza mwaka 2011 ikiwa na maono ya kuhakikisha hatokei mtoto akaugua au kufariki kwa saratani bila kupata tiba.

Pia, alisema dhima yao ni watoto wenye matatizo hayo wanapata huduma sahihi na yenye viwango vya kimataifa.

"Tukiwa Hospitali ya Ocean Road, tulikuwa na vitanda kama 17, lakini kwa sasa hapa Muhimbili vipo takriban 70, wadau wametusaidia kujenga hosteli hapa, ilijengwa kwa sababu watoto walikuwa wakipata dawa ilikuwa vigumu kumaliza mzunguko wa matibabu. "Tuliona badala kumruhusu aende nyumbani, anakaa hapa na mzazi au mlezi wake, ukifika muda wa kurudi wodini inakuwa rahisi."

Alisema upatikanaji wa huduma hizo umewawezesha kupandisha uwezo wa kuishi kwa watoto hao kwa asilimia zaidi ya 50.

Mongella alisema wamekuwa na wafadhili mbalimbali akiwamo taasisi ya MO ambayo kuanzia mwaka 2013 hadi sasa imekuwa ikitoka fedha za kuwasaidia watoto hao. Mkurugenzi wa Taasisi ya MO, Rachel Carp, alisema tangu mwaka 2013 wamesaidia Tumaini la Maisha ambacho ni kituo kikubwa cha saratani Afrika Mashariki.

Alisema kituo hicho kwa kushirikiana na Hospitali ya Muhimbili kinasaidia matibabu na huduma nyingine kwa watoto wenye saratani nchi nzima.

Alisema matibabu hayo ambayo ni ya hali ya juu hutolewa bure na maono ya Tumaini la Maisha yanahamasisha kuhakikisha kila mtoto mwenye saratani anapata nafasi ya kuishi.

Mkurugenzi wa Tiba Hospitali ya Muhimbili, Dk. Edwiga Swai, alisema kwa mwaka Hospitali ya Muhimbili inaona watoto wa saratani zaidi ya 2,000 na 600 wakiwa ni waliolazwa, 1,400 ni wagonjwa wa nje.

"Hospitali ya Muhimbili inahudumia watoto wa saratani Tanzania nzima, watoto chini ya miaka mitano wanatibiwa bure, lakini kwa misaada tunayopata kwa wafadhili wetu na MO Dewji ni mfadhili mkubwa, watoto wanatibiwa bila malipo yoyote.

"Matibabu ya saratani ni ghali, mtoto mmoja anaweza kutumia zaidi ya Sh. milioni 21, kwa misaada yenu watoto wetu wameendelea kuwa na hali nzuri, ukizingatia namba niliyotaja, asilimia 80 wanatoka mikoani na Watanzania wengi hatuna uwezo."

Swai alisema kwa misaada hiyo wanapata matibabu ikiwamo kupata chakula bure wao na wazazi au walezi wao hata wanapokuwa kipindi cha kusubiri katika hosteli ya Tumaini la Maisha iliyopo ndani ya hospitali hiyo. Alisema saratani za watoto nyingi zinatibika endapo dawa zinapatikana.

"Kwa sasa tunapata dawa kwa hiyo ile dhana mtoto wangu ana saratani atakufa imepungua kwa wazazi na walezi wa watoto hawa na uelewa umekuwa mkubwa," alisema.



# DE JONG

## AITABIRIA MAKUBWA BARCA

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Frenkie de Jong, amesema Barcelona inaenda kuwa timu bora sana msimu huu licha ya sakata la kiuchumi linaloikumba klabu hiyo.

Suala kubwa linalotawala vichwa vya habari juu ya Barcelona kwa sasa ni suala la fedha na kushindwa kwao kukamilisha usajili wa Lionel Messi mpaka sasa.

Lakini de Jong bado ana matumaini kuwa wapo kwenye njia sahihi na watakuwa bora zaidi msimu huu.

Licha ya sakata la kushindwa kukamilisha usajili wa Messi, kocha Ronald Koeman amepata kikosi chenye wachezaji wazuri na wenye vipaji kuelekea msimu mpya, wakiwamo Sergio Aguero, Memphis Depay, Eric Garcia na Emerson Royal kwenye sehemu ya kikosi hicho.

Licha ya masuala ya nje ya uwanja, Barcelona watahitaji kufanya kila liwezekanalo kujiboresha zaidi msimu huu.

Na De Jong ameliambia Marca; "Ninaamini kikosi kitakuwa bora zaidi kwenye msimu huu wa joto, tunaenda kuwa bora zaidi kama timu.

"Ni mwaka wa pili wa bosi (Ronald Koeman) ni kawaida kuwa bora kwenye mwaka wa pili. Ninadhani tutapata fursa ya kupambana na kushinda mataji muhimu msimu unaokuja."

# SHEVCHENKO AACHANA NA UKRAINE

**KYV, Ukraine**

KOCHA wa Ukraine, Andriy Shevchenko amemaliza mkataba wake na timu ya taifa, wiki chache baada ya kuiongoza nchi yake kwenye robo fainali ya Euro 2020.

Shevchenko aliteuliwa kuwa kocha wa Ukraine mnamo Julai, mwaka 2016 na ameiongoza jumla ya michezo 52, pamoja na michezo mitano kwenye Euro za msimu huu wa joto.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa AC Milan na Chelsea alitangaza kuondoka kwake kupitia kurasa yake ya Instagram, hapo jana.

"Nimetumia miaka mitano na timu ya taifa," aliandika Shevchenko kwenye Instagram.

"Kwa bidii tumeonyesha kuwa tuna uwezo wa kucheza mtindo wa kisasa wa mpira wa miguu.

"Asante kwa mashabiki wote kwa msaada wenu na ukosoaji. Tumeonyesha pamoja kwamba tunaweza kuwa na ushindani na kufurahi."

Shevchenko, ambaye alicheza mechi 111 kwa Ukraine, akifunga mabao 48 kati ya 1995-2012, alichezea klabu yake ya nyumbani ya Dynamo Kiev ambapo alishinda mataji matano ya ligi ya Ukraine kabla ya kujiunga na AC Milan kisha Chelsea.





# Arteta: White alikuwa kwenye mipango yetu

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema kuwa usajili wa nyota mpya ndani ya kikosi hicho ambaye ni Ben White ulikuwa ni mpango wa mabosi wa timu hiyo.

Nyota huyo ambaye ni beki amejiunga na timu hiyo akitoka Brighton ikiwa ni lengo la kuimarisha ulinzi ndani ya kikosi hicho kinachoshiriki Ligi Kuu England.

Ni dau la pauni milioni 50 limetumika kupata mkataba wa nyota huyo na imempa kandarasi ya miaka mitano kudumu ndani ya Arsenal na amepewa jezi namba nne.

Akiwa ndani ya Brighton msimu uliopita beki huyo alipiga jumla ya 'takolini' za uhakika kwa asilimia 53 katika mechi 36 za Ligi Kuu England.

Arteta amesema: "Ben kuja hapa ni mpango wetu wa muda mrefu kwenye kuongeza ulinzi. Ni beki mwenye akili nyingi katika eneo lake akiwa na mpira mguuni."

HABARI MICHEZO



# KANE AKATAA KURUDI SPURS

**LONDON, England**

HARRY Kane nyota wa Tottenham Hotspur amewaambia mabosi wake, kwamba hayupo tayari kuwa ndani ya timu hiyo kwa msimu ujao jambo ambalo linamfanya ahitaji kupata changamoto mpya.

Nyota huyo ambaye ni nahodha wa timu ya taifa ya England kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kuingia kwenye rada za Manchester City, Chelsea na Arsenal, ambao wanahitaji huduma yake.

Kwa mujibu wa Sky Sports ripoti zimeeleza Kane amewaambia mabosi wa timu yake, kwamba kwa msimu huu anahitaji kuondoka Spurs jambo ambalo linamfanya afungue njia kwenye timu nyingine, ambazo zinamhitaji.

Mwenyekiti wa City, Khaldoon Al Mubarak hivi karibuni alibainisha kwamba wanahitaji kusajili kikosi bora, ambacho kitakuwa na ushindani zaidi jambo ambalo linatoa nafasi kwao kuweza kumpata Kane ilikuwa ni baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tunahitaji kuwa kwenye ushindani na utayari kwa ajili ya msimu ujao. Kwa msimu huu tutaimarisha kikosi kwa kuleta wachezaji bora na wenye uwezo mkubwa,"

# BAJETI YA USAJILI UNITED HADHARANI

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inatarajia kuwauza baadhi ya wachezaji, ili kujiimarisha msimu huu, huku ikijiandaa kutumia pauni milioni 75 hadi 100, kwa mujibu wa ripoti.

Katika mpango huo United inataka kumuuza Paul Pogba kwa pauni milioni 50 na Jesse Lingard kwa pauni milioni 30 na mauzo hayo kutumika kumsajili kiungo na kupata saini ya Kieran Trippier.

Tayari uhamisho wa Jodon Sancho akitokea Borussia Dortmund kwa pauni milioni 73, umemekamilika na hivi karibuni United itatangaza kukamilisha usajili wa beki wa Real Madrid, Raphael Varane kwa pauni milioni 42.

Beki wa kulia wa Athletico Madrid, Trippier anatarajiwa kusajiliwa na United wiki kadhaa zijazo.

Lakini, usajili huo utategemea kwa kiasi kikubwa iwapo Pogba na Lingard wataruhusiwa kuondoka.

Hadi sasa bado haijulikani kuhusu majaliwa ya wawili hao, ingawa ripoti zinasema wanaweza kuuzwa wakati wowote.



# MARTIAL KUWA CHAMBO KWA HAALAND

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United iliripotiwa kuwa tayari kumuacha Anthony Martial aondoke klabuni hapo kwenye soko hili la msimu wa joto.

Taarifa zaidi za hivi karibuni zinabainisha kuwa United wanajiandaa kumtumia Martial kwenye dili la Earling Braut Haaland.

Chelsea wanatajwa kuongoza mbio za kuwania huduma ya Haaland, ambaye anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 150, ikiwa ataondoka msimu huu wa uhamisho.

Ripoti zinasema kuwa Dortmund hawana mpango na dili la kubadilishana wachezaji, na hivyo dau lililopo mezani ndiyo linaweza kuamua ni nani ataipata saini ya staa huyu.

Lakini, United wanajiandaa kuwashawishi Dortmund kumsaini Martial, ili kurahisisha biashara yao.

Mfaransa huyu alifanikiwa kucheka na nyavu mara nne tu kwa msimu uliopita na kutoa asisiti tatu.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer kwa sasa anatarajia kuzingatia ofa zinazoweza kuwasilishwa kwa ajili ya saini ya staa huyo mwenye umri wa miaka 25.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN ATAKA KUREJEA ATLETICO

**MADRID,** Hispania

**Lakini mazungumzo kati ya Barca na klabu yake hiyo ya zamani yanaonekana...**

NYOTA wa Barcelona, Antoine Griezmann ameripotiwa ana nia ya kutaka kurejea Atletico Madrid katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta amethibitisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anapatikana sokoni kwa uhamisho msimu huu wa joto wakati klabu hiyo ikisaka kuweka sawa vitabu vyao vya fedha.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia amehusishwa na kurejea Atletico kama sehemu ya makubaliano ya kubadilishana na nyota Sauli Niguez, lakini mabingwa hao wa LaLiga wameshindwa kufikia makubaliano na kikosi cha Ronald Koeman.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Griezmann yuko tayari kuondoka Camp Nou kwenye soko la sasa, lakini mshambuliaji huyo ana nia ya kuhamia Atletico Madrid.

Ripoti hiyo inadai klabu kadhaa za Ligi Kuu England na Serie A ziko tayari kumchukua kwa mkopo kwa msimu huu 2021-22, na kipengele cha uhamisho wa kudumu msimu ujao wa joto.

Hata hivyo, kocha wa Barcelona, Ronald Koeman majuzi alibainisha kwamba, anataka kuendelea na nyota huyo kwenye kikosi chake, kwani amekuwa na kiwango cha kuvuti kwenye kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya. Mfaransa huyo alifunga mabao 133 na kutoa asisti 50 katika mechi 257 za Atletico kati ya mwaka 2014 na 2019 kabla ya kuhamia Barcelona kwa dili la fedha nyingi.

Griezmann amejitahidi sana kuonyesha kiwango chake bora huko Camp Nou, akiweza kufunga mabao 35 na asisti 17 katika mechi 99 za klabu kwenye mashindano yote.

## KWA UFUPI

### KANE AIVURUGA CITY

MANCHESTER City wamepungukiwa na pauni milioni 40 kati ya pauni milioni 160 bei ambayo Tottenham inataka kumuuza mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. (***Star***)

### NI CHELSEA NA LUKAKU

CHELSEA hawajakata tamaa ya matumaini ya kumsajili tena mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, kutoka klabu ya Serie A ya Inter Milan. (***Athletic, subscription required***)

### MESSI SAFI BARCA

BARCELONA wako tayari kutangaza rasmi mkataba mpya wa miaka mitano wa mshambuliaji na nahodha wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34 katika siku chache zijazo. (***Sport***)

### RAMSEY ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wameuliza juu ya uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30. (***Goal***)

### UNITED YAMSUBIRI HAALAND

MANCHESTER United ina miezi 12 ya kumshawishi mshambuliaji wa Borussia Dortmund raia wa Norway, Erling Braut Haaland kwamba ni klabu sahihi kwake. Mchezaji huyo ambaye anasakwa na Chelsea na klabu nyingine, anatarajiwa kuhama katika msimu wa majira ya joto wa mwaka 2022 wakati klabu zitakapoweka kipengele cha kumwachilia cha takriban pauni milioni 75 kwenye mkataba wake wa Dortmund. (***Manchester Evening News***)

### VILLA YAREJEA KWA PROWSE

ASTON Villa wamewasilisha ofa ya pili kwa ajili ya kiungo wa kati wa Southampton, mwenye umri wa miaka 26, James Ward-Prowse baada ya ofa ya awali ya pauni milioni 25 kukataliwa. (***Mail***)

### ASENSIO AGEOMBEWA

KLABU za Leicester City, Leeds United na Everton zinashindana kumsajili winga wa Real Madrid Mhispania Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25. (***Fichajes***)

### TRIPPIER ANUKIA UNITED

ATLETICO Madrid wanajiandaa kwa uwezekano wa kumuuza mlinzi, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30 kwa klabu ya Manchester United ili kujiandaa kumchukua mchezaji wa Roma, Alessandro Florenzi mwenye umri wa miaka 30. (***AS***)

### SHEFFIELD SOKONI

KLABU ya Sheffield United ipo katika mazungumzo kwa ajili ya kuingia katika mkataba na kiungo wa kati wa kikosi cha zamani cha England, Ronaldo Vieira mwenye umri wa miaka 23, akitokea Sampdoria. (***Mail***)

### KAMARA MAMBO SAFI

NEWCASTLE United wanaangalia uwezekano wa kuingia mkataba na kiungo wa kati Mfaransa Boubacar Kamara mwenye umri wa miaka 21, kutoka Marseille kwa takriban pauni milioni 10. (***Mail***)

## HABARI MICHEZO

## LIGI YA WANAWAKE MWANZA YAKARIBIA

**Na Saada Akida**

LIGI ya Wanawake Mkoa wa Mwanza inatarajia kufanyika kuanzia Agosti 29, mwaka huu, imefahamika.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Mkoa wa Mwanza (TWFA- Mwanza), Sophia Makilagi alisema jana maandalizi ya ligi hiyo yamekamilika na wanatarajia msimu huu utakuwa na ushindani zaidi. Makilagi alisema timu zote zinazotarajia kushiriki kuendelea na maandalizi, ili bingwa atakayepatikana awe imara na atakayekwenda kuiwakilisha vizuri Mwanza katika Ligi ya Mabingwa ya Taifa (WRCL), itakayochezwa baadaye mwakani.

"Sisi kama viongozi wa mkoa tumejiandaa vizuri, mashindano haya yatakuwa endelevu, tunawaomba wadau wote wa soka la wanawake kujitokeza na kushirikiana vyema na timu zetu, ili kufikia malengo," alisema Makilagi.

Naye Katibu Mkuu wa TWFA-Mwanza, Revina Muzawena alisema chama chao kimelitangaza vyema soka la wanawake katika Mkoa huo kwa kuhamasisha kwenye kila wilaya.

Muzawena alisema wanaamini klabu zikiwa na nguvu, maendeleo ya soka la wanawake yatapatikana kwa urahisi na wao wamepania kupeperusha vyema Mkoa wao.

## POLISI TANZANIA YAMNASA TARIK

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA kiungo wa Biashara United ya Musoma, Tarik Simba amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuwatumikia 'Maafande' wa Polisi Tanzania kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa mchezaji huyo, Ahmad Kassim 'Prezidaa' alisema mchezaji huyo ameshasaini mkataba baada ya kumalizana na waajiriwa wake wa zamani wa Biashara United.

Prezidaa alisema amefurahishwa na namna pande zote mbili zilivyoendesha mazungumzo na anaupongeza uongozi wa Polisi Tanzania kwa uamuzi wa kumsajili mchezaji wake, ambaye amejiandaa kuisaidia timu hiyo katika msimu mpya.

"Polisi Tanzania walianza kumfuatilia kwa muda mrefu kiungo wangu kwa ajili ya kutaka huduma yake, ni kweli Tarik Simba amesaini mkataba wa miaka miwili akiwa mchezaji huru," alisema Prezidaa.

Naye Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Hassan Kayoza alisema nyota huyo na wengine walikuwa katika mipango yao na muda wowote huenda wakatangaza wachezaji wapya, ambao watawasajili.

# NYOTA WALIOREJEA AZAM WAFANYA VYEMA KAGAME

**Na Adam Fungamwangwo**

WACHEZAJI wa Azam waliokuwa wakicheza kwa mkopo katika klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita wameisaidia timu hiyo kuanza vyema katika mashindano ya Kombe la Kagame kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya mabingwa watetezi, KCCA kutoka Uganda.

Timu hizo zilikwenda mapumziko huku kila moja ikishindwa kuzitikisa nyavu za mwenzake katika mchezo huo wa Kundi B uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Azam imewarudisha wachezaji wake wote iliyowatoa kwa mkopo na sasa wanaitumikia timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Kagame.

Baadhi ya wachezaji hao ni Oscar Masai ambaye alikuwa akiichezea Ihefu, Idd Kipwagile aliyekuwa Namungo FC, Lusajo Mwaikenda, Masudi Abdallah na Paul Peter, ambao walikuwa wakiichezea KMC.

Katika mechi hiyo, Peter aliyekuwa KMC ndiyo aliyefunga mabao yote mawili.

Mbali na wachezaji hao, Azam pia ilichezesha baadhi ya wachezaji wa kikosi cha pili, pamoja na wale ambao hawakupata nafasi sana kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo akiwamo kiungo, Awesu Awesu.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia alisema lengo ni kuangalia wachezaji, ambao wako vizuri kuwarudisha kwenye kikosi cha kwanza na hatimaye msimu ujao kuwa na kikosi kipana.

**"Kama tulivyosema tumewarudisha baadhi ya wachezaji wetu waliokuwa wakicheza kwa mkopo na umeona faida yake. Wamecheza vizuri na kocha wetu (George Lwandamina), amepata nafasi ya kuwaona vizuri, sasa chaguo ni lake. Lengo ni kukifanya kikosi kiwe kipana, kwa sababu msimu ujao tutakuwa na mashindano mengi," alisema Zacharia.**

Azam itashuka tena dimbani kesho kuwavaa Le Messager Ngozi FC ya Burundi wakati mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wao watawakaribisha KCCA ya Uganda.

Michuano hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Big Bullets, kucheza dhidi ya Express ya Uganda wakati Atlabara ya Sudan Kusini itawavaa wenyeji Yanga, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

KCCA ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo inayosimamiwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ambacho kiko chini ya Rais, Wallace Karia.



Beki wa Azam FC, Bakari Abdilahi (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KCCA ya Uganda katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Kagame iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam, juzi usiku. Azam ilishinda mabao 2-0. PICHA: JUMANNE JUMA

## Siboka ajichimbia akiandaa albamu

**Na Sabato Kasika**

MSANII wa nyimbo za asili, ambaye ni kiongozi wa Kundi la Mfalme, Costa Siboka amesema yuko katika maandalizi ya albamu yake mpya, ambayo itazinduliwa hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili, Siboka alisema kwa sababu hiyo, amelazimika kusitisha maonyesho, ili kuendelea kujifua pia, wakijikinga na ugonjwa wa corona.

Siboka alisema kwa sasa anaendelea kurekodi nyimbo za albamu mpya ambayo haujapewa jina, pia akifanya utambulisho katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Kanda ya Ziwa.

"Kundi letu limeshakamilisha baadhi ya nyimbo mpya ambazo ni pamoja na Shikwamo, Mgulinde, Jitarhumba, Wawawa Remix, Kanchepe, Omwanga Wange na Mla Chake.

Aliongeza nyimbo hizo zitatambuliwa rasmi kwenye tamasha la Shangwe za Ukerewe Festival litakalofanyika Desemba, mwaka huu, ambapo itaambatana na utambulisho wa wacheza shoo wapya.

Siboka ambaye kundi lake huimba nyimbo za makabila mbalimbali ya kanda ya ziwa, alisema mbali na kuendelea na shughuli zake za muziki, anawahimiza wasanii wenzake kujitokeza kupata chanjo ya kujikinga na corona.

"Chanjo ndio mpango mzima, tujitokeze kama alivyotuongoza Rais wetu Mama Samia Suluhu," Siboka alisema.


# Michezo



Jumatano Agosti 4, 2021
Nipashe

## Griezmann ataka kurejea Atletico

HABARI UK. 22



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (kulia), akiwa na Mratibu wa Miradi na Masoko wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), Gabriel Nderumaki, wakionyesha nakala za mikataba ya haki za matangazo ya kurusha hewani mechi za Ligi Kuu Bara kwa upande wa redio iliyosainiwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

## TFF yazidi kuneemeka

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba wa haki ya matangazo ya urushaji wa mechi za Ligi Kuu Bara kwa upande wa redio na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), wenye thamani ya Sh. bilioni 3.5.

Rais wa TFF, Wallace Karia alisema mkataba huo utakuwa wa miaka 10 na shirika hilo litakuwa linaipatia shirikisho lake Sh. milioni 300 kwa kila mwaka, ambazo zitagawiwa sawa kwa klabu zote zitakazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Karia alisema kiasi kingine cha fedha kitapelekwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya soka nchini.

"Ninawapongeza TBC kwa kushinda tenda, ninaimani kuendesha mpira ni gharama, TFF itahakikisha klabu inapata gawio kwa ajili ya kuendesha timu zao, tunajua kuendesha mpira unahitaji fedha, viongozi wanatakiwa kuzitumia katika matumizi sahihi, kwa sasa ligi yetu iko kwenye nafasi nzuri, kwa Afrika tuko nafasi ya nane, hii ni jambo la kujivunia," alisema Karia.

Kiongozi huyo alisema katika ligi hakuna mkubwa, timu zote ziko sawa na mgao wote utakuwa sawa.

Naye Mratibu wa Miradi na Masoko wa TBC, Gabriel Nderumaki alisema wamefikia uamuzi huo, ili kuwapa nafasi ya Watanzania wengi kupata matangazo hayo ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa sababu ya mtandao mpana waliokuwa nayo ndani na nje ya nchi.

# MAKAMBO: NIMERUDI 'KUWAJAZA'

## Afunguka kurejesha mataji Yanga ambayo leo inawavaa Atlabara katika...

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Yanga umemtambulisha rasmi straika wake wa zamani, Heritier Makambo, ambaye amerejea klabuni hapo kwa ajili ya kuitumikia timu hiyo katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa 2021/22.

Yanga iliyomaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika na kufungwa katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA, itashiriki michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Makambo amesaini mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo inayofundishwa na Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi baada ya kutambulishwa, Makambo alisema kiwango chake ni kile kile kama alivyoondoka na ameahidi kutobadilisha staili yake ya ushangiliaji kama alivyokuwa akifanya alipokuwa na timu hiyo katika msimu wa 2018/19.

Makambo alisema amefurahi sana kupata nafasi nyingine ya kurejea Tanzania ambako anakufananisha sawa na nyumbani kwao.

"Nimefurahi kurudi tena. Hapa ni nyumbani. Nafurahi kuwaona Wana-Yanga wote. Kila siku nilikuwa naangalia, nasikiliza maoni yao wakinitaka nirudi Yanga, na kweli nimesikia na nimerejea," alisema Makambo.

Alisema anaamini kwa kushirikiana na wachezaji wenzake atahakikisha wanaipatia furaha timu yao, ambayo imeshindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu minne mfululizo.

"Makambo ni yule yule wanayemfahamu. Tutafanya kazi pamoja na wachezaji wenzangu kwa ajili ya kufurahisha mashabiki. Unajua Yanga ni timu kubwa na inatakiwa icheze kila msimu au kila mwaka kwa ajili ya kutafuta mataji. Nimerudi kupambana, ili kuchukua makombe," alisema Makambo ambaye alipotoka Yanga alikwenda kujiunga na Horoya ya Guinea kwa misimu miwili ya 2019/20 na 2020/21.

Straika huyo alisema mabadiliko ya muundo wa uendeshwaji ndani ya Yanga, pia yamechangia yeye kurejea tena katika timu hiyo, tofauti ilivyokuwa ikiendeshwa kabla ya kuondoka nchini.

Kuhusu staili yake ya kushangilia, alisema hatoibadilisha kwa sababu tayari ilishazoeleka na kuwa maarufu kwa wanachama na mashabiki wa Yanga, hivyo ataendelea nayo.

"Makambo ni yule yule na staili ya ushangiliaji nayo ni ile ile pia ya kuwajaza," Makambo alisema.

Makambo anakuwa straika wa pili wa kigeni kusajiliwa baada ya mabosi wa klabu hiyo kumtambulisha mshambuliaji mwingine, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Fiston Mayele.

Makambo ambaye aliichezea Yanga kwa msimu mmoja na kupachika mabao 17, msimu wa 2018/19, alisema kuwa kiwango chake ni kile kile tofauti na watu wanavyofikiria.

Naye Mayele alisema amefurahia kujiunga na Yanga na malengo yake ni kuisaidia timu hiyo ichukue ubingwa.

"Ninapenda kufanya kazi vizuri kama nilivyofanya katika timu niliyokuwa ninacheza, lengo langu ni kuona tunakuwa mabingwa, nitapambana katika kila mechi, ili kushinda, ninajua timu yetu ina malengo mengi, tutapambana ili kuyafikia," Mayele alisema.

Nyota wengine wapya waliosajiliwa na Yanga kwa ajili ya msimu ujao ni pamoja na Dickson Ambundo aliyekuwa Dodoma FC na Yusuph Athumani kutoka Biashara United.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa alisema wanaendelea kuimarisha kikosi chao kwa sababu wamedhamiria kutwaa mataji mbalimbali katika msimu huu mpya.

Mfikirwa alisema wanatarajia kufanya vizuri katika mechi ya leo dhidi ya Atlabara ya Sudan Kusini, ili wajiweke kwenye nafasi ya kusonga mbele.

"Tunalitaka kombe, hii ni klabu kubwa, huwezi ukashiriki ukiwa huna malengo, tunamalengo nao na tuna makusudi nao, timu yetu itakuwa inabadilika kulingana na mahitaji ya mechi, tunakwenda kucheza kesho (leo), ili kushinda, itakuwa ni fedheha kuliacha kombe liondoke," alisema Mfikirwa.

Mechi nyingine ya mashindano hayo ya Kundi A itakayochezwa leo ni kati ya Nyasa Big Bullets dhidi ya Express.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >